SUPA JACKPOT
TZS. 1,067,615,605
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 8

**SHEKHE** Ponda atoa neno uhuru wa vyombo vya habari nchini


Nipashe
TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
MVUA ZINAPOKOLEA
Zitumike kilimo na ufugaji, kupanda miti ya kutosha
Nivyo ulivyo umuhimu wa kuandikisha elimu ya awali
Utoro unapotishia kidato cha kwanza, wadau wataja mbinu kuukomesha
SAYANSI
NA MWANDISHI WETU
YANAFURAHISHA 2023
Ni kubadilisha seli kuondoa maradhi, udhaifu
•Chanjo kuzalishwa 'chap chap', kiufanisi zaidi

# Nipashe

Jumanne Januari 17, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581193
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

# MFUMUKO WA BEI







**SERIKALI** yamulika maeneo manne kuleta ahueni...

*Endelea ukurasa 2*



Mawasiliano ya eneo la Kona ya Mnyagara, Wilaya ya Tanganyika mkoani Rukwa yakiwa yamekatika na mvua na kusababisha usumbufu kwa watumiaji wa barabara hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizara tano ngumu safari hii kusalimika panga la Rais Samia?

UKURASA 3

UKURASA WA 7

## WAPEWA ANGALIZO UTUNZAJI SAMPULI WASHUKIWA WA TB

WATOA huduma za afya ngazi ya jamii wameonywa dhidi ya tabia ya kulala na sampuli za makohozi ya washukiwa wa ugonjwa wa kifua kikuu (TB) kwenye majumba yao ili kuziepusha familia zao kuambukizwa ugonjwa huo...

UKURASA WA 9

## SABA KATI YA 40 WARIPOTI KUANZA KIDATO CHA KWANZA

WANAFUNZI 33 kati ya 40 waliochaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari...

UKURASA WA 10

## JELA MAISHA KWA UDHALILISHAJI KIJINSIA

MKAZI wa Kidatu "B" Kata ya Mtendeni mkoani Tabora, Hussein Mashibu (32), amehukumiwa kwenda jela maisha kwa kosa la kumlawiti...



## PM aagiza ulinzi wa mbolea ya ruzuku

UKURASA 2

**MICHEZO** TALIB ASIFU USAJILI MPYA SIMBA UK. 23

**KATUNI** UK. 6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na wananchi wa Mbeya Mjini baada ya kuwasili mkoani humo kwa ziara ya kikazi katika mikoa ya Mbeya na Songwe jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Serikali yamulika maeneo manne kupunguza mfumuko wa bei

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imetaja maeneo manne yatakayoisaidia Tanzania kukabiliana na mfumuko wa bei na kuleta unafuu ili nchi isiathirike zaidi kiuchumi.

Aidha, imesema mfumuko wa bei utaendelea kuwapo kutokana na kutegemea uagizaji wa mafuta na mitambo kutoka mataifa makubwa ambayo pia yameathiriwa na mfumuko huo.

Hata hivyo, imeondoa hofu ya nchi kukabiliwa na upungufu wa chakula na kwamba pamoja na bei ya bidhaa kupanda imekuwa ikiendelea kuingilia kati kuhakikisha haiathiri mwananchi.

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru, alisema hayo alipokuwa akielezea hali ya uchumi wa dunia, fursa na athari zake kwa Tanzania, wakati akitoa mada kwenye mafunzo na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari, jijini Dar es Salaam, jana.

Alisema mfumuko wa bei umeyakumba pia mataifa makubwa duniani, ikiwamo Marekani, China na Umoja wa Ulaya baada ya janga la UVIKO-19 na kufuatia vita vya Urusi na Ukraine.

Akiyataja maeneo yatakayosaidia nchi kujiimarisha kiuchumi, alisema kuwa ni sekta ya utalii, kilimo, maliasili, gesi asilia na usafirishaji kutokana na eneo la kijiografia Tanzania ilipo.

Akifafanua kuhusu maeneo aliyoyataja, Mafuru alizungumzia sekta ya utalii ambayo Rais Samia Suluhu Hassan, alifanya juhudi kuitangaza kupitia filamu ya Royal Tour, baada ya kuathirika kutokana na ugonjwa wa UVIKO-19 ulioitikisa dunia na kusababisha watalii wengi kusitisha safari zao na kuathiri mtiririko wa fedha za kigeni.

Alisema sekta hiyo ni moja ya nguzo muhimu katika kulipatia taifa fedha za kigeni, watalii wanapoingia nchini kwa wingi.

Vile vile, akizungumzia kilimo, Mafuru alisema mikakati inapowekwa vizuri uzalishaji wa chakula utaongezeka na kutoa fursa ya kuuzwa ndani na nje ya nchi na pia kutokuwa na upungufu wa bidhaa hiyo.

Alisema Tanzania imejaliwa kuwa na maliasili nyingi zikiwamo za mafuta na gesi, madini ya dhahabu, nikel na makaa ya mawe ambao zinawezesha taifa kupata fedha za kigeni na kupunguza athari za mfumuko huo.

"Ombwe la kushuka kwa utalii nchini lilifidiwa na soko la dhahabu, ndiyo maana hatukupata athari kubwa kwenye fedha za kigeni...inaonesha jinsi gani sekta nyingine zinavyotulinda inapotokea janga," alisema Mafuru.

Alisema maliasili hizo zikifanikiwa kutumika vizuri kibiashara, nchi itakuwa imejikomboa kwa kupata unafuu wa mfumuko wa bei ambao ulimeiathiri dunia kwa sasa.

Kuhusu gesi asilia (LNG), alisema Tanzania ingefanikiwa kuanza kutumia mradi wake ingefaidika kwa kuiuza nchi nyingine na kutoa mfano wa nchi ya Msumbiji ambayo inapata manufaa kwa kuuza kama nishati mbadala baada ya mafuta kupanda bei kwenye soko la dunia.

"Tukiweza kutumia nishati mbadala ikiwamo gesi, solar, badala ya kutegemea umeme kwa kutumia mafuta, tutahifadhi fedha za kigeni," alisisitiza.

**MKAKATI KISERA**

Akielezea mwelekeo kwa taifa, Mafuru alisema mikakati ni kuweka sera zitakazowavutia wawekezaji wa nje kuwekeza nchini.

Aidha, alisema serikali inaendelea kushughulikia sera za kikodi ambazo sio rafiki, kutengeneza miundombinu wezeshi (ikiwamo barabara, umeme na maji) ili kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji na mikakati mizuri ya kifedha (kuvutia mitaji ya sekta binafsi).

**ATHARI VITA URUSI/UKRAINE KIUCHUMI**

Akizungumzia vita inayoendelea kati ya Urusi na Ukraine ilivyoathiri Tanzania, Mkurugenzi Utafiti Uchumi na Sera, Suleiman Missango kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), alisema nchi imeathirika kiuchumi kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta ambayo imepanda kwenye soko la dunia na kusababisha shughuli za uendeshaji pia kupanda.

Alisema bei ya mafuta inapopanda inagusa kila sekta, ikiwamo wasafirishaji, wauza bidhaa, chakula kupandisha gharama.

Alisema nchi za Urusi na Ukraine ni wazalishaji wakubwa wa ngano ambayo inategemewa na sehemu kubwa ya dunia, hali iliyosababisha bidhaa hiyo kupanda bei na kuathiri pia Tanzania.

Alishauri watu kujifunza kutumia bidhaa mbadala badala ya kutegemea mikate ambayo inatumia ngano na kupenda kula vitu vya asili kama mihogo, viazi na magimbi ambavyo hupatikana nchini na kwa bei nafuu.

# PM aagiza ulinzi mbolea ya ruzuku

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wananchi kuwa walinzi wa mbolea ya ruzuku iliyotolewa na serikali ili kuhakikisha inatumika kwa malengo yaliyokusudiwa ya kuongeza uzalishaji wa mazao katika msimu wa 2022/23.

Amesema kumekuwa na Watanzania wachache wasiokuwa na nia njema wanaotorosha mbolea kwenda nchi jirani na kuwaacha Watanzania bila kuwa na mbolea ya kutosha.

"Jambo hili lazima tulikemee na tulisimamie sote ili kuhakikisha mbolea iliyoko nchini, ni kwa ajili ya Watanzania, kila mmoja awe mlinzi kwa mwenzake," Majaliwa aliagiza alipowasalimia wananchi kwenye eneo la Mbalizi jijini Mbeya jana akiwa katika ziara ya kikazi ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa na serikali.

Alisema utoaji wa ruzuku hiyo ya mbolea unalenga kuongeza uzalishaji wa chakula nchini na ni marufuku kuiuza nje.

Aliongeza kuwa awali mbolea iliuzwa kwa zaidi ya Sh. 100,000 lakini serikali ikaridhia kutoa ruzuku Sh. bilioni 150 ili kushusha bei ya mbolea na sasa inauzwa kwa Sh. 70,000.

"Tusikubali fedha hiyo kutumika nje ya malengo, tulinde mbolea yetu isiuzwe kwa wasiohusika.

"Nimefurahi sana kwa hatua zilizochukuliwa mkoani Songwe, tani 2,199 zimekamatwa zikipelekwa nchi jirani, hii haikubaliki, Watanzania tuwe walinzi, hizi ni fedha zetu, zinatoroshwa na wachache, malengo yetu ni kuwahudumia ninyi kwa usimamizi wa Rais Samia," alihimiza.

Waziri Mkuu alitumia fursa hiyo kuelekeza hatua zilizofikiwa katika maendeleo ya uboreshwaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Songwe kuwa tayari njia ya kurukia ndege imekamilika kwa asilimia 100, jengo la abiria ujenzi umefikia asilimia 96 na sasa ufungaji taa unaendelea na ukikamilika, uwanja huo utaanza kutumika wakati wote.

"Tunafanya hivi ili kuvuta masoko kutoka nchi jirani ikiwamo Kongo, Zambia na Malawi walete ndege zao, haya yote yanafanywa na serikali kwa sababu ina maono ya mbali na dhamira ya dhati ya kuwaletea Watanzania maendeleo," alisema.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso alisema serikali imeidhinisha Sh. bilioni 3.3 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji wa Shongo-Igale ambao umekamilika na watu wanapata huduma.

Aliongeza kuwa licha ya mahitaji ya maji Mbalizi kuwa lita milioni nane, serikali ilitoa Sh. bilioni. 4.8 kwa ajili ya kujenga mradi wa maji wa Inunga ili kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni nane hadi 12.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais -TAMISEMI, David Silinde, alisema serikali imetenga Sh. milioni 580 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 29 kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambapo yote yamekamilika kwa asilimia 100 na yanatumika.

Baadhi ya wananchi walimwomba Waziri Mkuu awasaidie kulipwa fidia iliyotokana na kupisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe, wakisubiri malipo tangu mwaka 2002.

Hata hivyo, Meneja wa Uwanja huo, Danstan Komba alisema wanachodai wananchi hao ni mapunjo ya fidia.

Alisema kuwa baada ya eneo lao kutwaliwa, walilipwa fidia lakini baadaye yalitokea malalamiko ya mapunjo ya fidia ambapo timu ya uchunguzi ya suala hilo iliundwa na ilishafika kwenye eneo hilo, hivyo aliwaomba wananchi watulie wakati suala lao linaendelea kufanyiwa kazi.

# Wizara tano ngumu zitasalimika safari hii panga la Rais Samia?

**Na Restuta James**



NI wazi kwamba wakati joto la panga pangua ya Rais Samia Suluhu Hassan linaendelea kupanda, huku mawaziri wanaoongoza wizara zinazojulikana kuwa ni 'ngumu' wakiwa katika kitendawili cha kuvuka daraja hilo.

Tathmini ya Nipashe ambayo imeegemea zaidi rekodi za kihistoria, wizara hizo ni zile ambazo mawaziri wamekuwa wakihudumu kwa kipindi kifupi na ni nadra kutoguswa kila mabadiliko ya muundo wa Baraza la Mawaziri yanapofanyika.

Marejeo ya rekodi ya kihistoria yanagusa wizara za: Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI); Wizara ya Maliasili na Utalii; Elimu, Sayansi na

Teknolojia; Ujenzi na Uchukuzi; na Nishati.

Itakumbukwa kwamba mwaka 2015, Rais John Magufuli (Hayati) alipoingia madarakani, aliteua manaibu waziri kwenye baadhi ya wizara, pasipo kuteua mawaziri. Hata hivyo, akawateua mawaziri baadaye.

Kwa mujibu wa sheria nchini, mwenye mamlaka ya kuendesha wizara ni waziri kamili.

**KWANINI WIZARA NGUMU?**

TAMISEMI; inaangukia kwenye kundi hilo kwa sababu majukumu yake ya msingi yanagusa kila sekta, ikiwa na wajibu wa moja kwa moja wa kuwajibika kwa mwananchi aliko. Mathalani, zahanati kisera zinaratibiwa na Wizara ya Afya, lakini mmiliki na anayezihudumia ni TAMISEMI.

Wizara hiyo ngumu katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, imekwishaongozwa na mawaziri watatu ambao ni Ummy Mwalimu, Innocent Bashungwa na wa sasa Angellah Kairuki.

Inaporejewa historia ya nchi, wizara hiyo ilianzishwa na Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa (Hayati) ambayo Waziri mwasisi alidumu kwa muda mfupi.

Rais Magufuli alipoingia madarakani, alihamisha kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kwenda Ofisi yake, akisema inahitaji uangalizi wa karibu zaidi.

Taarifa zinaonyesha kuingia kwa Rais Samia madarakani Machi 2021, wizara ilianza na Ummy Mwalimu, aliyedumu kwa kipindi kifupi kabla ya kurithiwa na Innocent Bashungwa aliyekuwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Bashungwa akahudumu kwa miezi tisa kati ya Januari hadi Oktoba mwaka jana, kabla ya kuingia Angellah.

Kabla ya hapo, waziri aliyedumu zaidi katika wizara hiyo ni Dk. Seleman

Jafo, aliyekaa kwa miaka minne kuanzia 2017 hadi 2021.

**MALIASILI NA UTALII**

Ni wizara nyeti inayoingiza robo ya fedha za kigeni nchini na kuchangia asilimia 17.5 ya Pato la Taifa, pia ni kati ya wizara ambazo Rais Magufuli aliumiza kichwa kuteua mawaziri wake, hata ikachukua miezi kadhaa kupata waziri.

Rekodi za wizara hiyo, zinampa nafasi Daktari wa binadamu, Hamis Kigwangalla kwamba ndiye aliyedumu kwa kipindi kirefu zaidi tangu uongozi wa awamu ya tano hadi wa sasa, akikaa kati ya 2017 na 2020.

Pia, mrithi wake, mwanasheria Dk. Damas Ndumbaro alidumu kwa miaka miwili kati ya 2020 na 2022 alipomwachia kijiti Balozi Dk. Pindi Chana.

Ni wizara mlezi wa maeneo yaliyohifadhiwa kama Hifadhi za Taifa 22, mapori ya akiba, mapori tengefu, maeneo ya mtawanyiko na vitalu vya uwindaji wanyamapori.

**NISHATI/MADINI**

Nishati na Madini (sasa zimetenganishwa). Ni wizara zinazoshika hazina za taifa, maisha ya kawaida ya Watanzania, huku uendeshaji wake kila mara umekuwa ukiandamwa na kashfa.

Historia mojawapo iliyotikisa zaidi ya mulongo mmoja na nusu sasa ni kujiuzulu kwa Waziri Mkuu wa kwanza katika Serikali ya Awamu ya Nne, kupitia kilichojulikana kama 'Kashfa ya Richmond Mwaka 2008'.

Nchini katika Serikali ya Awamu ya Tano, alianza kuiongoza Mwanajiolojia Prof. Sospeter Muhongo mwaka 2015.

Naye hakubaki salama, alitikiswa na hata kulazimika kujiuzulu kutokana na kilichojulikana kama 'Kashfa ya Fedha za Akaunti ya Escrow' zilizokuwa zinabishaniwa kati ya Shirika la Umeme (TANESCO) na kampuni binafsi ya kufua umeme ya IPTL.

Prof. Muhongo baada ya kujiuzulu na kuonekana yuko salama, alirudishwa madarakani nako hakudumu sana, ndani ya miaka miwili tu, akang'oka baada ya wizara hiyo kugawanywa kupata wizara mbili; Nishati aliyokabidhiwa Dk. Medard Kalemani na Madini, Angellah Kairuki.

Angellah aliongoza kwa miaka miwili hadi 2019 alipompisha aliyekuwa msaidizi wake, Dk. Doto Biteko anayeiongoza hadi sasa.

Mtikisiko upande wa Sekta ya Nishati, ulimwangukia mwasisi Dk. Kalemani anayetajwa kuhudumu kwa muda mrefu kati ya 2017 na 2021.

Hapo uteuzi mpya ulimrejesha kundini aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, January Makamba aliyekuwa 'benchi' tangu mwaka 2019 uteuzi wake ulipotenguliwa katika Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira); anatumikia cheo hicho cha Nishati hadi sasa tangu 2021.

**WIZARA YA ELIMU**

Nayo inaingia kwenye orodha ya wizara zinazotajwa kuwa ngumu kutokana na kutoa huduma kwa sekta nyeti ya elimu inayoamua hatima ya malezi na ukuaji kitaaluma.

Hata hivyo, rekodi zinaonyesha katika miaka ya karibuni, mawaziri wanaoteuliwa wamedumu kwa kipindi kirefu kulinganishwa na miaka ya nyuma.

Wizara hii imeongozwa na Dk. Joyce Ndalichako aliyehudumu katika kipindi chote cha kwanza cha Rais Magufuli.

Rais Samia alimhamisha na nafasi yake kuchukuliwa na Prof. Adolf Mkenda.

**UJENZI, UCHUKUZI**

Kama ilivyokuwa kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi haikupata mapema waziri

kwenye awamu ya kwanza ya muundo wa Baraza la Mawaziri la Rais Magufuli, kipindi hicho ikiitwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Rais Magufuli alianza kwa kumteua Edwin Ngonyani kama Naibu Waziri. Ni wizara ambayo 'inaonekana' sana kutokana na kuwa na miradi mikubwa

ya ujenzi ya kimkakati ambayo inatumia mabilioni ya shilingi ya walipakodi.

Baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es

Salaam - Mwanza hadi Burundi, ununuzi wa mabehewa kwa ajili ya reli na Daraja la Magufuli.

Waziri wake wa sasa, Prof. Makame Mbarawa ni kama ana 'nyota' na

wizara hiyo kwani amehudumu kwa vipindi tofauti kwenye mabadiliko ya Baraza la Mawaziri.

Wakati wa muundo wa Baraza la Mawaziri la Rais Magufuli, Prof. Mbarawa alipelekwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, alikohudumu kwa siku 11 kabla ya kurudishwa Wizara ya Ujenzi kuiongoza.

Akihutubia kwenye mkutano mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) uliofanyika hivi karibuni jijini Dodoma, Rais Samia alisema anatarajia kufanya mabadiliko ya serikali yake ili kupata viongozi watakaoendana na kasi yake.

Baada ya kauli hiyo, Januari 3 mwaka huu Rais Samia alimteua Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa (TISS), Diwani Athumani kuwa Katibu Mkuu Ikulu, nafasi iliyokuwa inashikiliwa na Moses Kusiluka ambaye aliteuliwa Katibu Mkuu Kiongozi. Saa chache baadaye, uteuzi wa Athumani ulitenguliwa.

Tangu wakati huo kumekuwa na mjadala mrefu kwenye mitandao ya kijamii huku wengine wakibashiri mabadiliko kwa kuweka picha na majina ya watu wanaodaiwa kushika nafasi za juu serikalini.

# Vyoo chakavu vyatishia usalama wa wanafunzi

**Na Asraji Mvungi,** KONDOA

UHABA wa matundu ya vyoo na uchakavu wa miundombinu umelalamikiwa kutishia usalama wa maisha ya wanafunzi kwenye Shule ya Msingi Ihari iliyoko Kijiji cha Ihari, Kata ya Busi wilayani Kondoa mkoani Dodoma.

Mkuu wa Shule hiyo, Mwalimu Matokeo Ngoitanile, alibainisha hayo juzi shuleni huko alipozungumza na waandishi wa habari waliotembelea shule hiyo na kuwaomba wadau kuwasaidia.

Kwa mujibu wa Mwalimu Ngoitanile, shule hiyo sasa ina wanafunzi 715 wanaotumia matundu manane ya vyoo, sawa wastani wa wanafunzi 89 kwa tundu na yaliyoko hali yake ni mbaya kutokana na uchakavu.

"Hapa tuna tatizo kubwa sana la miundombinu kuanzia vyoo, madarasa na nyumba za walimu. Miundombinu hii ni ya zamani sana na imechoka na kwa kweli msaada wa haraka unahitajika," alisema Mwalimu Ngoitanile.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ihari, Rumishael Moshi, alisema tatizo hilo linachangiwa kwa kiasi kikubwa na mwamko mdogo wa wananchi kuchangia maendeleo unaosababishwa na ukata unaowakabili.

"Asilimia kubwa ya wananchi hapa ni wakulima ambao kwa sasa wameathiriwa kwa kiasi kikubwa na mabadiliko ya tabianchi, jambo linalosababisha uchangiaji wa maendeleo kuwa mgumu, lakini bado tunaendelea kupambana kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali na baadhi yao wameanza kusaidia.

"Baadhi ya wadau walioanza kujitolea kusaidia kutatua tatizo hilo ni watendaji wa Pori la Akiba Mkungunero lililoko jirani na kijiji hicho ambao wametoa misaada vifaa kwa ajili ya kuboresha baadhi ya miundombinu ya shule hiyo.

Akizungumzia wakati wa kukabidhi baadhi ya vifaa hivyo yakiwamo mabati, saruji, mbao na vifaa vingine, Kamanda wa Uhifadhi wa Pori la Mkungunero, Floravicky Kalambo alisema msaada huo ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yao kwa kuwa pamoja na majukumu yao ya msingi ya kusimamia uhifadhi, pia wanawajibika kusaidia wananchi wanaoishi jirani.

"Sisi kama TAWA tulibaini tatizo hili wakati tukiwa katika majukumu yetu ya kutembelea vijiji jirani kutoa elimu kwa wananchi ya umuhimu wa uhifadhi na tukaingiza tatizo hilo kwenye mipango yetu na leo tumeanza utekelezaji," alisema. Kwa mujibu wa Floravicky, wataendelea kusaidia utatuzi wa tatizo hilo kadri watakavyoweza na pia kusaidiana na wananchi wa vijiji vyote jirani katika masuala ya maendeleo.

Diwani wa Busi, Madina Athumani aliwashukuru wadau hao kwa msaada huo na kuwaomba wengine kuona umuhimu wa kusaidia.

Madina pia aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa kudumisha uhifadhi ambao sasa wanaona matunda yake.



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sauti ya Mama Afrika (SAMAFO), Tabitha Bugali (kushoto), akikabidhi msaada wa nguo kwa Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Maafa Mkoa wa Mbeya, Erick Sichinga juzi, kwa ajili ya waathirika wa mafuriko ya mvua iliyonyesha wiki iliyopita. Wengine ni viongozi wa serikali wa mkoa huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## RC awataka wafanyabiashara kuchangamkia fursa Comoro

**Na John Badi**

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Ahmed Abbas, amewaomba wafanyabiashara mkoani humo kuchangamkia fursa za kibiashara baina ya mkoa huo na nchi jirani ikiwamo Comoro.

Pia ameipongeza Benki ya Exim Tanzania kwa kuwa mstari wa mbele kufanikisha huduma za kifedha baina ya Tanzania na visiwa hivyo.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa tawi jipya la Benki ya Exim mkoani Mtwara, Kanali Abbas alisema kuwa licha ya kuwapo fursa za biashara kutokana na mahitaji ya bidhaa za chakula, ikiwamo maharage, nyama, ulezi na ufuta Comoro, changamoto ilibaki kuwa ni huduma za kifedha baina ya mataifa hayo mawili.

Alisema jitihada za Benki ya Exim kuboresha huduma hizo zitatatua changamoto hiyo.

"Nimefurahi kusikia kwamba Benki ya Exim ina matawi zaidi ya matano Comoro na ndiyo benki inayoongoza kwa ukubwa Comoro na leo (jana) hii tunazindua tawi lao jipya na la kisasa zaidi hapa Mtwara.

"Jitihada hizi za Exim ndiyo zinanipa nguvu ya kuwashawishi zaidi wafanyabiashara mkoani Mtwara na maeneo jirani kutumia vyema fursa hii kwa kuwa uhakika wa huduma za kifedha sasa upo... tunawashukuru sana Benki ya Exim," alipongeza.

Kwa mujibu wa Kanali Abbas, uzinduzi wa tawi hilo umekuja wakati mwafaka, kipindi ambacho mkoa huo unatarajia ugeni wa viongozi wakubwa kutoka Comoro watakaoambatana na idadi kubwa ya wafanyabiashara kutoka nchini humo, wanaokuja kujionea fursa za biashara baina ya mataifa mawili.

Akizungumza kwenye ya hafla hiyo, Mkuu wa Idara ya Mtandao wa Wateja wa Benki ya Exim, Agnes Kaganda, alisema uamuzi wa kuboresha zaidi tawi hilo unalenga kuunga mkono jitihada za serikali za kukuza uchumi wa mkoa huo.

Alisema kuwa kupitia uwekezaji mkubwa kwenye upanuzi wa huduma za bandari na kuboresha hali ya kilimo, kunachochea ukuaji wa biashara ya ndani na ile ya kimataifa hususani kati ya Tanzania na Comoro.

"Baada ya kuona jitihada hizo za serikali na kwa kuheshimu wateja wetu, tukaona ni vyema tuwafungulie tawi lenye hadhi wanayostahili.

"Tawi hili pia linaendana na mabadiliko makubwa ya huduma za kisasa za kibenki zinazohusisha matumizi ya teknolojia ya hali ya juu katika utoaji wa huduma za kifedha," alisema.

"Kupitia huduma hii isiyo na mipaka, raia wa Comoro anayetembelea Tanzania kwa sababu za biashara, matibabu au madhumuni yoyote, anaweza kutoa fedha au kufanya malipo ya huduma hizo wakati wowote akiwa nchini bila kuathiriwa na sababu za kimipaka baina ya mataifa haya mawili," alifafanua.

Akizungumza kwa niaba ya wateja wengine wa benki hiyo mkoani Mtwara, Henry Shimo, aliiomba benki hiyo kuendelea kuboresha upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu zaidi kwa wakazi wa mkoa huo wanaotegemea kilimo, uvuvi na biashara ili wanufaike zaidi na jiografia ya mkoa huo unaopakana na mataifa ya Msumbiji na Comoro.

## SAMAFO yawapa msaada waathirika mafuriko

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Sauti ya Mama Afrika Foundation (SAMAFO) mkoani Mbeya imetoa msaada wa nguo kwa ajili ya waathirika wa mafuriko kwenye Kata za Iduda, Uyole, Iganjo, Nsalaga na Igawilo yaliyotokana na mvua ilizonyesha Januari 7, mwaka huu na kusababisha madhara makubwa.

Akikabidhi msaada huo, mbele ya kamati ndogo ya maafa mkoani Mbeya, Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Tabitha Bugali, alisema wameamua kutoa msaada huo baada ya kuguswa na kusikia taarifa kwenye vyombo vya habari.

Alisema kuwa baada ya kupata taarifa za mafuriko, walilazimika kukusanya nguo za watoto za kiume na kike kwa ajili ya kusaidia waathirika ambao ni wakazi wa kata hizo.

Katibu wa SAMAFO, Hidaya Marekani aliwashukuru wanachama waliochangia msaada huo, ambao wameuwasilisha mkoani humo kwa ajili ya kusaidia waathiriwa hao.

Akipokea msaada huo, Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Maafa mkoani Mbeya, Erick Sichinga aliishukuru taasisi hiyo kwa namna ilivyojitokeza kutoa msaada huo, akibainisha kuwa bado kuna uhitaji mkubwa wa msaada kwa jamii hiyo iliyokumbwa na maafa.

Alisema misaada yote inapokewa na kamati hiyo na itashirikiana na kamati mama inayoongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya ambaye atakabidhi wilayani ili kuwafikia walengwa.

Sichinga alitoa wito kwa taasisi na mashirika, kujitokeza kutoa msaada wa hali na mali ili kukabiliana na maafa kwa kuwa mvua inaendelea kunyesha.

Katibu wa kamati hiyo mkoani Mbeya, Juma Maduhu alisema kamati yake haipokei fedha taslimu, bali hupokea vitu na vyakula ambavyo vitatolewa kwa utaratibu maalum utakaopangwa na kamati mama.

Ofisa Tawala Mkoa wa Mbeya, Mohammed Mkindi, alisema msaada umekuja kwa wakati na utasaidia kupunguza makali kwa waathiriwa wa mafuriko.

Mafuriko hayo yalisababisha baadhi ya kaya kukosa makazi na vyakula huku vifaa vya wanafunzi vikiharibiwa.

Kata ya Uyole ndiyo iliyopata athari kubwa zaidi na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alitoa msaada wa chakula na kushauri kuboreshwa miundombinu husan mitaro jijini Mbeya.

# Kesi Kocha wa Makipa Simba yarudishwa kwenye upelelezi

**Na Grace Gurisha**

KESI ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroine kilo 34.89 inayomkabili aliyekuwa Kocha wa Makipa wa Klabu ya Soka ya Simba, Mwalami Sultan na wenzake watano, imerudishwa katika hatua za upelelezi baada ya upande wa mashtaka kupata taarifa zingine za kesi hiyo.

Januari 2, mwaka huu, upande wa mashtaka uliiarifu Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kwamba upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na umeshapeleka taarifa Mahakama Kuu.

Hata hivyo, Wakili wa Serikali Caroline Matemu, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate kuwa kuna taarifa wamepata kuhusiana na kesi hiyo, hivyo wanazifanyia kazi.

Kutokana na hali hiyo, Wakili Matemu alidai kesi hiyo imerudishwa katika hatua ya upelelezi na pia hatua ya kuwasilisha Mahakama Kuu taarifa imesitishwa.

Hakimu Kabate aliahirisha kesi hiyo ambayo ilikuwa ikiendeshwa kwa njia ya mtandao hadi Januari 30, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa na upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika kutokana na taarifa inayofanyiwa kazi.

Mbali na Sultan, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Mmiliki wa Kituo cha Soka cha Kambiasso Sports Academy, Kambi Seif, Maulid Mzungu, Said Matwiko, John John na Saraha Eliud.

Awali Wakili Matemu alidai kuwa upelelezi umekamilika na wameshapeleka taarifa Mahakama Kuu na kilichokuwa kinasubiri ni taarifa hiyo kurudishwa ili wawasomee washtakiwa maelezo ya mashahidi wa kesi hiyo.

Katika hati ya mashtaka, inadaiwa kuwa Oktoba 27, 2022, eneo la Kivule, ndani ya Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, washtakiwa walikutwa wakisafirisha kilo 27.1 za dawa za kulevya aina ya herione.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Novemba 4, 2022, huko Kamegele, Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, washtakiwa walikutwa wakisafirisha kilo 7.79 za dawa za kulevya aina ya heroine.

Washtakiwa hawakuruhusiwa kujibu kitu chochote mahakamani huko kwa kuwa Mahakama ya Kisutu haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

## Watumishi wa benki kortini madai wizi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

WATUHUMIWA saba, wakiwamo wa Benki ya NMB wilayani Igunga mkoani Tabora, wamepandishwa kizimbani kwa tuhuma za kughushi na kuiba zaidi ya Sh. milioni 60.

Watu hao walisomewa mashtaka hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Mkoa wa Tabora, Gabriel Ngaije.

Watuhumiwa hao wanakabiliwa na mashtaka matatu ambayo wanadaiwa kuyatenda kwenye benki hiyo wilayani Igunga.

Wakili wa Serikali, Robert Kumwembe, alidai mahakamani huko kuwa watuhumiwa walitenda makosa matatu ambayo ni kughushi nyaraka, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kughushi risiti za kuonyesha fedha zinazoingizwa kwenye akaunti ya mteja wao, Kija Dotto ni halali.

Watumishi wa Benki ya NMB waliofikishwa mahakamani ni Ngolo Lunengu, Ally Saidi, Prisca Shula, Sedalia Venance, Anastazia Richard, Boniface Henry na Anastazia Felix.

Kumwembe alidai watuhumiwa hao wanakabiliwa na kesi ya jinai ambayo waliitenda mwaka 2022 kwenye Benki ya NMB wilayani Igunga mkoani Tabora.

Watuhumiwa hao walipewa dhamana na kesi hiyo iliahirishwa hadi Februari 13, mwaka huu.

**Watuhumiwa hao wanakabiliwa na mashtaka matatu ambayo wanadaiwa kuyatenda kwenye benki hiyo wilayani Igunga.**



Meneja Mkuu wa Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, Cheick Sangare (kushoto) na Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Migodini na Kazi za Ujenzi (TAMICO), Paternus Rwechungura (katikati), wakitia saini makubaliano ya mkataba wa hali bora kazini katika hafla iliyofanyika Bulyanhulu, (kulia) ni Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgodi na wafanyakazi waingia makubaliano kuboresha maslahi

**Na Philemon Lusekelo**

MGODI wa Dhahabu wa Barrick Bulyanhulu ulioko Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga umeingia makubaliano ya hiari ya hali bora kazini na wafanyakazi wake.

Hafla ya kutia saini makubaliano hayo ilifanyika mwishoni mwa wiki kwenye mgodi huo na kushuhudiwa na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, upande wa mgodi ukiwasilishwa na Meneja Mkuu wa Mgodi huo, Cheick Sangare.

Wafanyakazi waliwakilishwa na Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Migodini na Kazi za Ujenzi (TAMICO), Paternus Rwechungura.

Akizungumza katika hafla hiyo, Katibu Mkuu wa TAMICO, Rwechungura, alisema makubaliano hayo yamefanikiwa baada ya mazungumzo ya muda mrefu kati ya menejimenti ya mgodi na TAMICO.

Alisema makubaliano hayo yamelenga kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa Barrick kwa kuwapa stahiki zao, mafao baada ya kustaafu kazi na fedha za motisha kwa ajili ya kusomesha watoto wa wafanyakazi.

Alieleza kuwa makubaliano ya Mkataba wa Hali Bora ni hatua ya utekelezaji wa sheria za kazi hususani Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Na.6 ambayo imeweka mazingira wezeshi ya kisera, kisheria na kitaasisi baina wafanyakazi na waajiri kwa lengo la kuboresha mazingira bora ya kazi, maslahi ya wafanyakazi na kuleta tija mahala pa kazi.

Rwechungura alisema amefurahishwa kuona uongozi wa mgodi umeona umuhimu wa makubaliano hayo ambayo kwa kiasi kikubwa yataongeza morali ya kazi kutokana na kukuza uhusiano mwema kazini.

Meneja Mkuu wa Mgodi huo, Cheick Sangare, alisema kutiwa sainiwa kwa makubaliano hayo ni kielelezo tosha cha mgodi huo kwenda kuyafanyia kazi makubaliano hayo kwa mujibu wa sheria huku akiwataka wafanyakazi kutimiza wajibu wao.

"Tumekubaliana pande zote mbili kuboresha maslahi, jambo ambalo sisi tutazingatia hilo na kutoka kwenu wafanyakazi tunategemea kuona mnaongeza juhudi na ubunifu katika kufanya kazi ili tupate wote manufaa katika kuongeza uzalishaji," alisema Sangare.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Kiswaga, aliupongeza mgodi huo kwa kuridhia makubaliano hayo ambayo pia yataongeza maslahi ya wafanyakazi na kuongeza Pato la Serikali kupitia kodi ya mshahara inayotozwa na Mamlaka ya Mapato (TRA).

Kiswaga alitumia nafasi hiyo kuwataka wafanyakazi kuongeza juhudi katika uzalishaji wa madini ili kupandisha pato la mgodi kwa kuuza dhahabu nyingi kwenye soko la dunia la madini hayo.

Hafla hiyo pia ilishuhudiwa na Kamishna wa Kazi Msaidizi, Andrew Mwalwisi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ambaye mbali na kupongeza kufikiwa kwa mkataba huo, pia aliwataka waajiri wote nchini kuzingatia kulipa viwango vipya vya mishahara, kikiwamo kima cha chini cha mshahara kilichotangazwa na serikali.

Alisema kima cha chini cha mshahara kimepanda lakini kumekuwa na tabia ya baadhi ya waajiri katika kampuni binafsi na umma kupuuza takwa la kisheria la kulipa viwango vilivyoelekezwa na serikali.

Mwenyekiti wa Tawi la TAMICO Mgodi wa Bulyanhulu, Maghembe Malimi, alipongea hatua hiyo na kuahidi kuwa wafanyakazi wako tayari kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuongeza uzalishaji wa dhahabu kwenye mgodi huo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Matukio yanayodhalilisha watoto lazima hatua zichukuliwe kudhibiti

**MATUKIO** ya ukatili dhidi ya watoto yanazidi kushika kasi huku baadhi yao wakifundishwa vitendo vibaya ambavyo haipaswi kuzungumzwa na kuachwa bila hatua madhubuti na mkakati wa kuwanusuru kuchukuliwa.

Matukio yanayoripotiwa ni watoto wa kiume kuharibiwa na watu wa karibu, marafiki, ndugu au na wanafunzi wenzao huku wakitishiwa kuuawa wakitoa siri. Katika ripoti maalumu iliyoripotiwa kwenye gazeti hili jana, shule moja mkoani Kilimanjaro ambayo waathirika wa matukio hayo ya kikatili, walieleza uhalisia huku wazazi waliopeleka watoto wao shule binafsi za bweni wakieleza namna walivyogundua watoto wao wakifanyiwa unyama huo na wenzao wakubwa.

Vitendo hivyo vinawasononesha wazazi kutokana na watoto kuogopa kuwaeleza wanachofanyiwa mpaka mzazi anapoona utofauti na kumdadisi mwanawe ndipo anapogundua kuwa anafundishwa na mtu aliyepewa jukumu la kumwangalia akiwa shuleni ili awe salama, lakini badala yake yeye ndiye anayemharibu.

Mmoja wa watoto waliofanyiwa unyama huo alifichukua kuwa walikuwa wakipewa zawadi mbalimbali ikiwamo kalamu na penseli pamoja na kupewa fursa ya kuzungumza na wazazi kwa simu wanapopata shida. Chakusikitisha zaidi, watoto hao wanaofanyiwa unyama huo wanadai kupewa mafuta maalumu ya kufanyia vitendo hivyo na wavulana wa darasa la sita na saba, huku wakishawishi kwa muda mrefu kukubali kutendewa vitendo hivyo.

Huyo ni mmoja wa wazazi aliyekubali kueleza kwa uwazi, lakini baadhi ya shule hata za kutwa kumekuwa kukiripotiwa matukio hayo ambayo hufanyika kwa usiri mkubwa huku kizazi kikiendelea kuangamia.

Hivi karibuni shule moja wanafunzi walipewa karatasi wakaambiwa waandike jambo wanalochukia, watatu kati ya zaidi ya 400 waliandika wanachukia vitendo vya kufanyiwa kinyume na maumbile wanavyofanyiwa na wanafunzi wenzao.

Tunahitaji ushiriki wa jamii yote kuanzia wazazi, viongozi wa dini, serikali na jamii kwa ujumla kukabiliana na matukio haya ambayo yanaangamiza watoto na kuingiza utamaduni mpya kwa Watanzania.

Kwa sasa mzigo wa lawama unashushwa kwa wazazi kwamba wamekuwa wakitafuta fedha zaidi huku wakiacha mzigo wa malezi kwa wasichana wa kazi, jambo ambalo halikubaliki na wanapaswa kuweka mkakati wa kutimiza wajibu wa malezi.

Pia baadhi ya wazazi wanapeleka watoto shule za bweni kutokana na majukumu, kuishi eneo la mbali zaidi au kuepuka usumbufu wa wasaidizi wa nyumbani, lakini baadhi ya wazazi hawana ukaribu na watoto wao jambo linalotoa nafasi wafanyiwe vitendo hivyo.

Mungu aliumba mwanamume na mwanamke, kila mmoja aliumbwa kwasababu maalum na kupewa majukumu yake kimwili kwamba anayebeba mimba na kuzaa ni mwanamke, lakini sasa tunaona mahusiano ya kimapenzi kati ya mwanamke na mwanamke na mwanamume kwa mwanamume. Bila jamii kuchukua hatua hali itakuwa mbaya, vitendo hivi wanafanyiwa watoto wadogo ambao bado hawajajitambua, wanakuwa wakifanyiwa matendo hayo hadi wanakuwa watu wazima, baadaye idadi ya mashoga inaongezeka.


Ni muhimu serikali ikaweka mkakati madhubuti ambao utakuwa shirikishi wa kupinga vitendo hivi ambavyo kwa mila zetu havikubaliki kabisa, lazima kuwapo ufuatiliaji wa karibu kwenye shule hizi kwamba ukaguzi ufanyike usiku na mchana ili kudhibiti matukio haya.

Tunaamini ikiwa wakaguzi wa elimu watazitembelea shule na kuwapa wanafunzi nafasi ya siri kueleza mambo wasiyoyapenda yanayoendelea kwenye shule zao, wangeeleza mengi sana ambayo huenda wasingeyajua na ingekuwa rahisi kufuatilia na kukomesha.

Wanafunzi wana mambo mengi sana ikiwa watapewa nafasi ya kueleza yale wanayoyapitia na kuhakikishiwa usiri mkubwa, lakini nafasi haijapatikana ndio maana shule binafsi zinatajwa kama eneo linaloharibu wanafunzi.

Tupinge ukatili huu kwa nguvu zote vinginevyo jamii yote italia kilio cha kusaga meno.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mabinti fursa TEHAMA hizo

Na Sabato Kasika

**KATIKA** juhudi za kukuza ubunifu, ili kukabiliana na vikwazo mbalimbali vya maendeleo vinavyohitaji sayansi na teknolojia, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), kwa muda inaandaa mpango wa kuibua vipaji vya ubunifu kwenye Teknolojia ya Habari na Mawasiliano - TEHAMA kutoka kwa vijana wabunifu.

Mpango huo unalenga kuwashindanisha wabunifu wa vitu mbalimbali ikiwamo ya mifumo ya TEHAMA kusaidia kutatua vikwazo vinayoibuliwa ndani ya jamii ili kufanikisha maendeleo.

Hata hivyo, wakati kukiwa na juhudi za kuhamasisha vijana kuwa wabunifu katika TEHAMA, inaelezwa kuwa wasichana bado wako nyuma, kwenye kuchangamkia ubunifu.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, anasema takwimu mbalimbali zinaonyesha kuwa ushiriki wa mabinti na wanawake katika matumizi ya TEHAMA si mzuri, barani Afrika asilimia 24 tu ya wanawake wanashiriki kwenye TEHAMA, wanaume wakiwa ni asilimia 35.

Anafafanua kuwa, watu wanaosoma ' sayansi ya kompyuta' na mambo yanayohusiana na TEHAMA, wanawake ni asilimia 10 pekee na kwamba ni muhimu kuendelea kuongeza nguvu katika kupunguza pengo hilo.

Ninaunga na Nnauye katika wito wake wa kutaka kupunguza pengo hilo, kwa kuhamasisha mabinti na wanawake kujitokeza kwa wingi ili kuonyesha vipaji vyao vya ubunifu katika TEHAMA.

Hatua hiyo inaweza kusaidia nchi kuwa na wabunifu wengi wa jinsi zote, badala ya kuwa na kundi kubwa la wabunifu wa kiume, huku lingine likiendelea kubaki nyuma bila sababu ya msingi. Mapinduzi ya matumizi ya TEHAMA, yanalenga kuzalisha vijana wa kiume na wa kike wabunifu wa masuala ya teknolojia hiyo, watakaosaidia jamii na taifa kwa ujumla kwenda na wakati hasa katika hii ya sayansi na teknolojia.

Kwa kuwa kuupitia ubunifu katika TEHAMA, Tanzania imeendelea kung'ara kwenye mashindano ya ubunifu, ni wazi kwamba nchi ina vijana wenye uwezo mkubwa wa kufanya maajabu kupitia sayansi na teknolojia.

Hivyo ni vyema wasing'are wa kiume tu bali wote, hasa kwa kuzingatia kwamba wana uwezo sawa wa kufanya maajabu katika ubunifu katika teknolojia ya habari na mawasiliano bila kujali jinsi zao.

Mwaka jana Tanzania iling'ara katika mashindano ya ubunifu barani Afrika ya Umoja wa Mawasiliano ya Simu wa Afrika (ATU) ikizipiku nchi nyingi za Afrika katika ubunifu wa TEHAMA.

Mashindano hayo yenye kaulimbiu ya "mazingira bora yanayochagiza ubunifu wa TEHAMA kwa vijana," Tanzania iking'ara kwa washiriki Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Open University of Tanzania).

Washiriki wengine walikuwa ni Chuo Kikuu cha St. Joseph Tanzania ambao waliweka rekodi katika ukanda wa Afrika Mashariki, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ikiwa mratibu wa mashindano hayo.

Vijana wengine wameibuka washindi wa pili na kupata medali ya fedha katika mashindano ya kwanza ya Global Robotics Challenge nchini Uswisi na kushirikisha mataifa zaidi ya 190.

Ushindi huo ndio unaomfanya Nnauye kutaka mabinti na wanawake kujitokeza kwa wingi kushiriki katika ubunifu kwenye teknolojia hiyo angalau kuwa na uwiano badala ya kuwa na vijana wengi wa kiume.

Kwa kuwa serikali imeshaahidi kuendelea kufuatilia maendeleo ya wabunifu na kuona namna ya kuendeleza vipaji vyao, ahadi hiyo ingekuwa ni chachu kwa mabinti kuungana na wenzao wa kume kuwa wabunifu. Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaelekezwa kuandaa mpango wa kuwa na vituo vya ubunifu katika ngazi za mikoa na wilaya mbalimbali ili kusaidia kuinua vipaji vya vijana.

Hivyo, fursa hiyo isiwe kwa vijana wa kiume pekee bali wa kike nao waichangamkie, ili waweze kuonyesha vipaji vyao kwa kubuni vitu mbalimbali kwa maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

## Balozi: Marekebisho Sera ya China kuhusu UVIKO-19 yamekuja muda mwafaka

**BEIJING,** CHINA

MAREKEBISHO ya hivi karibuni ya Sera ya China ya kuzuia na kudhibiti janga la UVIKO-19 yamefanyika katika muda mwafaka na kupokewa vyema duniani kote, ikiwa ni pamoja na Tanzania, Balozi wa Tanzania China, Mbelwa Kairuki amesema katika mahojiano na Shirika la Habari la China, Xinhua.

China hivi karibuni iliboresha hatua zake za kukabiliana na UVIKO-19, kwa kupunguza usimamizi wake wa UVIKO-19 kutoka kutumia hatua za ugonjwa hatari wa kuambukiza Daraja A hadi Daraja B na kuhamisha juhudi za mwitikio kutoka kwenye maambukizi hadi kutunza afya na kuzuia maambukizi makali.

"Umekuwa uamuzi uliochukuliwa kwa muda mwafaka kwa sababu baada ya miaka mitatu, China imepata uzoefu wa kutosha, maarifa ya kisayansi na utaalamu wa kukabiliana na UVIKO-19," alisema Balozi Kairuki katika mahojiano hayo jana.

Aliongeza kuwa muda wa kuainisha tena virusi ni mwafaka kwa sababu jamii ya sasa ya virusi vya UVIKO-19 havisababishi ugonjwa mkali na vifo.

Kwa mujibu wa hatua zilizochukuliwa za kudhibiti UVIKO-19 kwa kutumia hatua za magonjwa hatari ya kuambukiza Daraja B, idara husika zimepanga na kutoa hatua za mpito kuhusu usafiri wa kuvuka mipaka.

Balozi Kairuki alisema hatua za mpito za kurahisisha usafari wa kuvuka mipaka zimepokewa vyema Tanzania na duniani kote.

"Sasa tunatarajia kuanza tena kwa usafiri wa watu kwenda na kutoka China," Balozi Kairuki alisema na kuongeza:

"Tuna matumaini kwamba uboreshaji wa Sera za China za kuingia na kutoka utasababisha utulivu wa minyororo ya kimataifa ya viwanda na ugavi na utasaidia kupunguza mdororo wa uchumi wa dunia."

Katika siku za hivi karibuni, baadhi ya nchi ziliweka vizuizi vinavyolenga wasafiri wanaowasili kutoka China, vikihusisha kupima virusi mara wanapoingia kwenye nchi husika na kuwekwa karantini kwa wale ambao wamepimwa na kukutwa na maambukizi. Balozi Kairuki alisema kuwa katika jitihada za kukabiliana na UVIKO-19, kila serikali duniani inabidi ilinde raia wake kwa kuyapa kipaumbele maisha ya watu kwa kutumia mbinu mahususi za kisayansi.

"Kama kuna somo moja ambalo tulipata kutoka kwenye janga la UVIKO-19, ni ukweli kwamba virusi havibagui," alisema mwanadiplomasia huyo.

Balozi Kairuki alisema China imekuwa ikiunga mkono kwa dhati Serikali ya Tanzania katika kukabiliana na janga la UVIKO-19. Kupitia msaada kutoka China na nchi nyingine rafiki, Tanzania imechanja chanjo dhidi ya UVIKO-19 kwa asilimia 40 ya wakazi wake. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2022, jumla ya dozi milioni 5.61 za chanjo dhidi ya UVIKO-19 zilizotolewa na China zilipokewa na Tanzania.

"Mwaka 2023, tutashuhudia kuongezeka kwa ushirikiano kati ya Tanzania na China kutokana na marekebisho ya hivi karibuni ya Sera ya China ya kuzuia na kudhibiti maambukizi, kutakuwa na shughuli nyingi za kiuchumi kati ya nchi hizo mbili," alisema.

Balozi Kairuki aliongeza: "Mwaka huu tutashuhudia kuongezeka kwa usafiri wa ndege za abiria na mizigo wa moja kwa moja kutoka Tanzania hadi China kupitia Kampuni ya Ndege la Tanzania (ATCL) na tunatarajia kurejea kwa kasi kwa usafiri wa watalii kutoka China hadi Tanzania."



Mkuu wa Mkoa Singida, Peter Serukamba, akimtwisha ndoo ya maji mkazi wa kijiji jana baada ya kuzindua miradi mitatu ya maji kwenye vijiji vya Kaselya, Zinziligi na Maluga yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.4 wilayani Iramba. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wapewa angalizo utunzaji sampuli washukiwa wa TB

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WATOA huduma za afya ngazi ya jamii wameonywa dhidi ya tabia ya kulala na sampuli za makohozi ya washukiwa wa ugonjwa wa kifua kikuu (TB) kwenye majumba yao ili kuziepusha familia zao kuambukizwa ugonjwa huo.

Mratibu wa TB na Ukoma wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, Dk. Mkasange Kihongole, alitoa angalizo hilo jana alipozungumza na kikosi kazi cha watoa huduma hao wakati wa kikao kazi cha kufanya tathmini ya kutambua mafanikio na vikwazo walivyopitia mwaka uliopita kilichofanyika mjini hapa.

Dk. Kihongole alisema taarifa alizonazo zinabainisha wapo watoa huduma wengi ambao wamekuwa wakilala na sampuli hizo majumbani mwao badala ya kuzipeleka kwenye zahanati na vituo vya afya ili zikahifadhiwe huko baada ya kuwa wamezichukua kutoka kwa washukiwa wanaowapa huduma.

Alisema kinachomsikitisha zaidi, wapo watoa huduma ambao wamekuwa wakizibeba sampuli hizo kwenye mifuko ya nguo zao, hali ambayo inatishia pia usalama wa afya zao.

Alisema endapo watoa huduma hao hawatabadilika na kuendelea na tabia hizo, upo uwezekano wa familia zao kupata ugonjwa huo, jambo ambalo ni hatari kwa afya zao na familia zao.

"Mkishapata hizo sampuli kwa washukiwa, mzipeleke zahanati na vituo vya afya vilivyoko jirani na maeneo yenu kwani ndiko kwenye vifaa vya kutunzia sampuli zote kwa usalama," alisisitiza Dt. Kihongole.

Awali akitoa taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha mwaka 2022, mratibu huo alibainisha kuwa halmashauri ilijipangia malengo ya kuibua wagonjwa 841 kwa mwaka na mfadhili aliwasilisha malengo yake kwa watoa huduma.

Akizungumzia taarifa ya utekelezaji kwa mwaka 2023, Dk. Kihongole alisema kuwa kwa kipindi hicho Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru imejipangia kuwafikia wateja 840 sawa na kila robo wawe wameibua wagonjwa 210 ambapo kwa idadi ya watoa huduma 40 waliopo kila mhudumu mmoja awe ameibua wagonjwa wasiopungua watano.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, watoa huduma hao, wakiwamo wa Kata ya Nandembo, Mungummoja Hyera na Mau Hasani wa Kata ya Misechela, walisema katika utekelezaji wa majukumu hayo, hufanya kazi kwa kutumia mikutano na mikusanyiko mbalimbali, wakiongea na washukiwa hao.

Walisema kuwa baada ya kubaini kuwapo viashiria, huendelea kuwafuatilia majumbani mwao ili kupata taarifa zaidi kwa familia zao na baadaye huwashauri wakapime na ikitokea amegundulika kuwa na ugonjwa huo, huwapeleka hospitalini kwa ajili ya kuanzishiwa dawa.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Shekhe Ponda atia neno uhuru vyombo vya habari

**Na Mwandishi Wetu**

SHEKHE Ponda Issa, Katibu wa Jumuiya na Taasisi za Kiislam Tanzania, amesema kuna haja serikali kuhakikisha vyombo vya habari vinakuwa huru ili kuviwezesha kufichua 'madudu' yanayofanywa na watendaji serikalini.

Akizungumza na waandishi jana jijini Dar es Salaam, Shekhe alisema uhuru wa vyombo vya habari ni msaada mkubwa kwa serikali yoyote duniani na kwamba si kila habari sahihi, Rais anaweza kuipata kutoka kwa wasaidizi wake wa Ikulu au serikalini.

"Nitatoa mfano wa gazeti la MwanaHalisi ambalo lilikuwa linafanya habari za uchunguzi, lilikuwa msaada mkubwa katika serikali ya awamu ya nne. Kulikuwa na habari ambazo yeye mwenyewe (Rais) ninaamini alianza kuzisoma pale na kisha kufuatilia. Si MwanaHalisi pekee, yapo na magazeti mengine pia.

"Wakati ule uhuru ulikuwapo ingawa si kwa kiwango stahili, lakini vyombo vya habari vilisaidia sana nchi katika kufukua habari zilizofanywa gizani. Hakuna namna nyepesi ya kuongoza nchi kama kuruhusu vyombo vya habari kufanya kazi yake kwa weledi unaolindwa na sheria rafiki, utamaduni wa vyombo vya habari kufanya kazi yake vizuri ulizimwa mwaka 2016," Shekhe Ponda alidai.

Kiongozi huyo na mwanazuoni wa Kiislamu, alisema ni vyema serikali sasa ikahakikisha mtoa taarifa za siri kwa vyombo vya habari kwa manufaa ya umma, analindwa kisheria. "Hapa sizungumzii siri za serikali katika utendaji wake, ninazungumzia siri za ubadhirifu. Katika nchi siyo kila jambo linapaswa kwenda kwa wananchi, ikiwa ni pamoja na masuala ya usalama wa taifa, jeshini na hata ndani ya wizara.

"Lakini kuna masuala ya wizi kupitia tenda mbalimbali, mikataba ya ovyo na hata ubadhirifu katika manispaa zetu ama balozi za nje ya nchi. Katika hilo kunapaswa kuwa na sheria inayolinda usiri wa mtoa taarifa za namna hii.

"Ukiwa na vyombo vya habari huru, vinavyofanya kazi bila kukandamizwa na dola, huwa na mchango mkubwa katika kupata taarifa sahihi sehemu ambapo labda vyombo vya serikali havijafika. Taarifa huru za vyombo vya habari, ni chanzo muhimu cha kunyoosha nchi," alisema.

Shekhe Ponda pia alitoa mfano inapotokea uamuzi wa mahamama kutoheshimiwa, akisema kuwa pale mahakama inapoamua jambo lake kuhusu chombo cha habari na serikali kutotekeleza, inatengeneza utamaduni wenye sumu katika siku za baadaye.

"Kuna baadhi ya mashauri yaliamuliwa na mahakama lakini Sheria ya Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 ikatumika vibaya kupinga haki hiyo.

"Mfano, kuna gazeti moja lilishinda kesi, lakini serikali ikanyima kibali cha kuendelea na kazi. Sheria zetu zisilenge kukomoa. Unapolifungia gazeti, tafsiri ya kwanza unaharibu uchumi wa gazeti hilo, unaharibu uchumi wa waandishi na wafanyakazi wengine wa gazeti hilo.

"Pia unahujumu mapato ya serikali kwa kuwa gazeti hilo linalipa kodi na wafanyakazi wake pia wanalipa kodi. Haya mambo ni vizuri serikali ikayaangalia kwa kuwa, hayaleti afya katika nchi," alishauri.



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Ahmed Abbas (wa pili kulia), akijiandaa kukata utepe kuashiria uzinduzi wa tawi jipya la Benki ya Exim mkoani Mtwara lililohamishiwa katika jengo la Sokoine House (PSSSF) katikati ya Manispaa ya Mtwara. Wanaoshuhudia ni Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya (kulia) na Mkuu wa Idara ya Mtandao wa Wateja wa Exim, Agnes Kaganda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Walimu wakumbushwa usafi wa mazingira

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Singida imewaagiza wakuu wa shule, walimu wakuu na maofisa elimu Kata na walimu kuzingatia suala la usafi kwa mtu binafsi, wanafunzi na mazingira ya shule ili kupendezesha madhari ya shule.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Jeshi Lupembe, alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na viongozi hao kwenye kikao cha kupitia mikakati ya uboreshaji na usimamizi wa elimu kwenye Manispaa ya Singida.

Alisema walimu wahakikishe wanatimiza wajibu wao katika majukumu yao ili kuitendea haki serikali iliyowapa madaraka.

"Nidhamu ya mtu binafsi katika kazi ndiyo msingi wa mafanikio katika uboreshaji elimu ambayo itachangia kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi shuleni, lazima tuibebe Singida kwa kila mmoja kutimiza wajibu wake," aliagiza.

Lupembe pia alihimiza walimu kusimamizi vizuri fedha na miradi inayopelekwa kwenye shule zao ili kuwasaidia wanafunzi kujisomea katika hali ya utulivu, pia kupendezesha madhari ya shule.

Pia aliwataka walimu kujali na kutumia vizuri muda, hasa muda wa ziada baada ya kazi kwa kufanya shughuli mbalimbali za kujiingizia kipato ili kujiandalia mazingira mazuri baada ya kustaafu. Kaimu Mkurugenzi huyo alitumia nafasi hiyo kuelezea baadhi ya mafanikio ambayo Manispaa ya Singida imeyapata kwa mwaka 2022 ikiwa ni pamoja na kusajili shule mpya tano za msingi, kujenga shule tatu mpya za sekondari, moja ikiwa ni ya kidato cha tano na sita.

Mafanikio mengine ni kujenga na kukamilisha kwa wakati vyumba 50 vya madarasa ambavyo serikali ilitoa Sh. bilioni moja na ujenzi wa kituo kipya cha afya Kata ya Mtipa kwa fedha za ndani. Ofisa Elimu wa Shule za Msingi, Omar Maje, aliwataka wakuu wa shule, walimu wakuu na maofisa elimu kata kubadilika na kuacha kufanya kazi kwa mazoea ili kuleta mabadiliko katika sekta ya elimu.

Maje alisema serikali imeanzisha utaratibu wa ujazaji mikataba kwa viongozi wa shule ili kuwafanya viongozi hao kuacha tabia ya kufanya kazi kwa mazoea na kujikita katika kuboresha elimu ili kuleta matokeo chanya.

Alisema kupitia utaratibu huo wa mkataba, wakuu wa shule, walimu wakuu na maofisa elimu kata, watasimamia maeneo yao ipasavyo na hivyo kufanya mabadiliko makubwa katika maeneo yao ya kazi.

# TAWA yatoa ufafanuzi tembo kuvamia makazi

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

UDHIBITI wa wanyamapori wakali na waharibifu unafanywa kwa kuzingatia mkakati wa kitaifa wa kutatua migongano baina ya binadamu na wanyamapori wa mwaka 2020-2024.

Mhifadhi Mkuu Uhusiano kwa Umma wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Vicky Kamata, alibainisha hayo juzi alipotoa ufafanuzi wa udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu baada ya taarifa iliyomhusisha Mbunge wa Mvomero, Jonas Van Zeeland, kuhusu kuwapo tembo eneo la Lubungo wilayani Mvomero.

Alisema taarifa hiyo iliyowasilishwa kwenye mkutano wa Waziri wa Maji, Juma Aweso, wiki iliyopita, iliwashutumu askari wa TAWA kutofanya kazi ya kudhibiti tembo waharibifu katika Wilaya ya Mvomero, akibainisha mkakati huo unaotekelezwa na wadau mbalimbali kwa kushirikiana ili kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu. Vicky alisema udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu kwenye Wilaya ya Mvomero siyo jukumu la TAWA peke yake, bali unafanywa kwa ushirikiano na taasisi zingine za uhifadhi, likiwamo Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kupitia Hifadhi ya Taifa Mikumi (MINAPA), Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero na wananchi wengine wote kwa ujumla.

"TAWA kwa kushirikiana na TANAPA na Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero waligawiwa maeneo ya kiutendaji ili kutoa huduma kwa wananchi katika Wilaya ya Mvomero kwa wakati, TAWA ilipewa kata sita za Lubungo, Melela, Wami Dakawa, Mlali, Mzumbe, Homboza na Sungaji na Hifadhi ya Taifa Mikumi walipewa kata tatu za Doma, Msongozi na Mangae," alifafanua.

Alibainisha kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero alitoa askari wanyamapori ili kushirikiana na askari wa hifadhi katika kudhibiti wanyamapori waharibifu hususan tembo na kwamba katika kukabiliana na changamoto wilayani humo, kwa kipindi cha Oktoba 2020 hadi Desemba 2022 kulikuwa na jitihada mbalimbali.

Alizitaja baadhi ya jitihada hizo kuwa ni doria za kudhibiti wanyamapori hao ambapo jumla ya siku 3,284 za doria zilifanyika dhidi ya matukio 264 yaliyotolewa taarifa kwenye Wilaya ya Mvomero, ikiwamo Kata ya Lubungo na Tarafa ya Mlali.

"Watu 4,151 walipewa elimu ya namna bora ya kuepuka madhara yanayosababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu hususan tembo. Mamlaka imejenga kituo cha askari wa kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kikiwa na pikipiki nne na gari moja kwenye Kijiji cha Sangasanga ili kurahisisha askari kufika kwa haraka kwenye matukio kabla tembo hawajaleta madhara," alisema.

Vicky aliongeza kuwa Kata ya Lubungo, jumla ya tembo wanne hatarishi walivunwa kwenye Kijiji cha Lubungo miongoni mwake wawili walivunwa mwaka 2021 na wengine wawili mwaka 2022. "TAWA wataendelea kuwa mstari wa mbele kuimarisha ulinzi wa maisha ya watu na mali zao kwa kuchukua hatua stahiki ili kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori katika vijiji vya Wilaya ya Mvomero na maeneo mengine nchini," alisema.

Alitoa wito kwa wananchi kupiga simu za dharura za kuripoti matukio hayo na kuacha kuwachokoza au kuwapiga wanyamapori pale wanapowaona kwenye makazi yao ili kuepuka madhara zaidi kwa wananchi. Mbunge Van Zeeland katika Mkutano wa Waziri wa Maji mapema Januari mwaka huu, alisema anafahamu changamoto ya tembo ambayo alishaiwasilisha kwa waziri mwenye dhamana bungeni lakini bado suala hilo halijapatiwa ufumbuzi na kuendelea kuwatesa wakazi wa kata nzima ya Mlali, ambao hawana uwezo wa kulima na wengine kuuawa na tembo.

Wiki iliyopita, mjini Bagamoyo mkoani Pwani, Meneja Ufuatiliaji na Tathmini wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), alibainisha kutokea vifo vya watu 1,069 na wengine 642 kujeruhiwa kutokana na migogoro ya binadamu na wanyamapori nchini katika kipindi cha miaka saba kuanzia 2012 hadi 2019.





## Trilioni 1.5/- zatengwa kujenga madarasa ya awali, msingi

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anayeshughulikia elimu, Dk. Charles Msonde, amesema serikali inatarajia kutumia Sh. trilioni 1.5 kujenga madarasa ya awali na msingi ili kuboresha elimu kupitia mradi wa boost.

Dk. Msonde alitangaza neema hiyo wakati akizungumza na walimu wakuu, maofisa elimu kata, maofisa elimu wa wilaya na mkoa wa Mkoa wa Manyara.

Alisema fedha hizo zimetolewa na Benki ya Dunia (WB) kwa ajili ya kuboresha madarasa ya awali na msingi ili kuwajengea msingi mzuri.

"Mwaka huu tunauanza kivingine kwenye sekta ya elimu usimamizi, uadilifu na uzalendo ndio tunavitaka,"alisema Dk. Msonde.

Aidha, alisema mwaka huu hawataki kusikia mwanafunzi wa darasa la awali mwaka mzima hajui chochote au mwanafunzi wa darasa la kwanza kupanda darasa bila kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Dk. Msonde alisema hadi kufikia Desemba mwaka jana, uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali na msingi ulikuwa asilimia 75.

"Tuhamasishe mtaa kwa mtaa au kijiji kwa kijiji, nyumba kwa nyumba ili uandikishaji ukamilike hadi Januari 31 na asibaki mtoto yeyote,"alisisitiza.

Kuhusu chakula kwa wanafunzi alisema siyo hiari tena ni suala la lazima kwa kuwa linasaidia kuboresha elimu kwa mwanafunzi.

Aidha, aliwaomba walimu, wazazi na walezi kuhakikisha watoto wanakuwa salama nyumbani, shuleni na njiani wanaporudi kutoka shule.

Dk. Msonde alisema suala la unyanyasaji wa watoto shuleni, nyumbani au njiani halikubaliki tena, kwamba hatua zinapaswa kuchukuliwa ili kuwalinda watoto.

Katika kikao hicho, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Joseph Mandoo, alisema ni vizuri halmashauri na serikali za vijiji zikatunga sheria ndogo ili kuwabana wazazi wachangie chakula cha wanafunzi.

# Saba kati ya 40 waripoti kuanza kidato cha kwanza

**Na Jaliwason Jasson,** SIMANJIRO

WANAFUNZI 33 kati ya 40 waliochaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Kitwai iliyoko Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, wamekwama kuripoti kutokana na kile kinachoelezwa ni kukosa sare za shule.

Shule hiyo ambayo ni ya serikali kati ya wanafunzi 40 waliochaguliwa kujiunga nayo ni wanafunzi saba pekee ndiyo walioripoti shuleni hadi sasa.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera, alisema walioripoti katika shule hiyo ni wavulana watatu na wasichana wanne.

"Kutokana na hali ninayoiona, naagiza wenyeviti wote wa vijiji na kata kuwafuatilia wanafunzi wapya wote wanaopaswa kuripoti mapema shuleni.

"Hata wale walioandikishwa shuleni waendelee kufuatiliwa nyumbani. Sitaki kisingizio chochote," alisema Dk. Serera.

Aidha, Dk. Serera aliagiza mwanafunzi yeyote wa kidato cha kwanza au shule ya msingi asirudishwe nyumbani kwa sababu ya kukosa sare za shule.

Alisema serikali imetoa ruhusa hiyo kwa wazazi na walezi, ambao hawajawashonea sare watoto wao ili wasiwe nyuma kimasomo.

"Tumefanya hivyo ili waanze masomo kwa wakati na pasiwe na kisingizio chochote kwani tumeruhusu wanafunzi kupokelewa wasio na sare wakikamilisha huku wakiendelea na masomo yao shueni," alisema Dk. Serera.

Kabla ya kutembelea Sekondari ya Kitwai, pia alikagua shule nyingine za Sekondari ya Loondrekes, Lormorijoi na Simanjiro.

Alisema wataendelea kutembelea shule nyingine ili kujionea uhalisia na kuchukua hatua kwa wale ambao kwa makusudi hawatatekeleza agizo la kuwapeleka watoto wao shuleni kama inavyoelekezwa na sheria na sera ya elimu.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mirerani, Tenisia Katukuru, alisema mwitikio wa wazazi na walezi kupeleka watoto wao shuleni ni mkubwa kwani wanatekeleza wajibu wao ipasavyo.



Askari wa Jeshi la Polisi mkoani Manyara wakifanya mazoezi wiki iliyopita kwenye Siku ya Mapinduzi ya Zanzibar wakiongozwa na Kamanda wa Polisi mkoani humo, Kamishna Msaidizi wa Polisi, George Katabazi, katika uwanja wa polisi. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Tozo ya utalii wa kitamaduni yawaliza wakazi Eyasi

**Na Allan Isack,** KARATU

WANANCHI wa Tarafa ya Eyasi, Wilaya ya Karatu mkoani Arusha, wamelalamikia tozo ya Dola ya Marekani 25 inayotozwa na Halmashauri ya Wilaya hiyo kwa ajili ya shughuli za utalii wa kitamaduni.

Shughuli za kitamaduni katika eneo hilo zinafanywa na jamii za Wadzabe, Wadatoga na Wahunzi.

Akizungumza jana kuhusu tozo hiyo, Kono Thomas, aliiomba serikali kuingilia kati na kusitisha tozo hiyo.

"Hiyo tozo haina uwiano sawa kati ya fedha zinazotozwa kama ushuru na zinazotolewa kwa walengwa.

"Tunaomba malalamiko yetu yamfikie Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa Halmashauri ya Karatu imetuchosha hatukukaa nao wala kupanga bei ila wenyewe wametupangia wakati sisi ndiyo wahusika na wadau wa utalii na tukiwauliza majibu yao wanasema kila mgeni anatakiwa kutozwa Dola ya Marekani 25 kwa kichwa.

Zaidi aliongeza: "Tunajiuliza ile Dola za Marekani 110 inakuwa imepotelea wapi kwa kuwa wageni 20 kwa Dola za Marekani 25 inakuwa ni Dola 500 hivyo hakuna mgeni atakayekubali kutoa kiasi hicho cha fedha kuja kuangalia utamaduni wa kabila letu." Alisema halmashauri hiyo itapata fedha nyingi kupitia kwa jamii hizo lakini wanawapangia viwango badala ya kukaa nao chini kusikiliza wahusika badala wa kuwapatia Dola za Marekani mbili ambazo haziwasaidii kitu chochote.

Aidha, Sainga Bashkey kutoka jamii ya Watatoga alisema wamesikitishwa na kitendo cha Halmashauri ya Wilaya hiyo kuwapangia bei bila ya kuwashirikisha walengwa kwa kuwa kiwango hicho ni kikubwa na kinawaumiza.

Alisema endapo halmashauri ikitaka kufanya mabadiliko hayo ya bei inapaswa kuwashirikisha walenga ili wakubaliane kwanza.

Kiongozi wa waongoza utalii wa kitamaduni Bonde la Ziwa Eyasi, Joseph Awe, alisema kero inayowakabili ni kuongezewa bei kwa kila mgeni atakayekwenda kutembelea jamii hizo atatakiwa kulipa Dola za Marekani 25 kama kiingilio.

Alisema kiingilio hicho ni tofauti na fedha za kufanya kazi ikiwamo kutembelea maboma na kumlipa mwongozaji wa watalii anayewapeleka watalii kuangalia utamatuni wao.

"Fedha hizo mwanzo zilikuwa zinanufaisha jamii kama mfuko wa maendeleo jamii ikiwamo kwenye matumizi ya matibabu, chakula na kuwapeleka watoto shuleni, lakini kutokana na utaratibu mpya wa mpangilio wa fedha hizo haziwezi kukidhi gharama za maisha za wananchi,"alisema Awe.

Akijibu malalamiko hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Karatu, Karia Rajabu, alisema kuwekwa kwa tozo hizo zitakuwa na manufaa kwa kuwa zitawasaidia jamii hizo.

Alisema: "Hicho kinachofanyika ni kwa ajilii ya kusaidia jamii hizo, lakini kuna baadhi ya waongoza utalii wanaharibu na kuwasumbua wananchi kwa maslahi yao binafsi ambayo hayako kwenye utaratibu".



# Ahukumiwa kwenda jela maisha kwa kulawiti

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKAZI wa Kidatu "B" Kata ya Mtendeni mkoani Tabora, Hussein Mashibu (32), amehukumiwa kwenda jela maisha kwa kosa la kumlawiti mwanaume (jina limehifadhiwa) hadharani.

Akitoa hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Tabora, Sigwa Mzige, alisema mtuhumiwa alipatikana na kosa la kumlawiti mtu mzima mwenzake ambaye ni mwanaume Januari 30, mwaka jana eneo la Kidatu B. mkoani Tabora.

Hakimu Mzige alisema mtuhumiwa alishtakiwa kwa makosa mawili ya kulawiti na kujeruhi kwa kumpiga na kitu kichwani na kumsababishia jeraha na kwamba makosa hayo yanakwenda pamoja na adhabu ya kulipa faini ya Sh. milioni moja.

Hakimu Mzige akitoa hukumu hiyo pasipo kuacha shaka baada ya ushahidi uliotolewa mahakamani hapo na watu watatu.

Watu hao ni mtuhumiwa mwenyewe, daktari ambaye alithibitisha kutokana na vipimo vya aliyelawitiwa ambavyo vilionyesha michubuko pamoja na mama yake.

"Mahakama zote nchini zinafanyakazi vizuri kuhakikisha kila mtuhumiwa analetwa hapa kwa makosa mbalimbali kila kosa moja lina adhabu yake," alisema Mzige.

Awali Wakili wa Serikali, Robert Kumwembe, aliiambia mahakama hiyo kwamba mshtakiwa ni mkosaji wa mara ya kwanza na anastahili adhabu hiyo ya kwenda jela maisha.

Mtuhumiwa huyo katika utetezi wake aliiambia mahakama hiyo kuwa alipata tetesi kwamba mtu huyo ana mahusiano na mke wake na siku hiyo alimfumania wakiwa wote ndani.

Hivyo aliiomba mahakama hiyo kumpunguzia adhabu hiyo kwa kuwa ana familia ya watu sita na mke wake kalazwa katika Hospitali ya Rufani Kitete kwa ajili ya kujifungua.

Hata hivyo, mahakama ilikataa ombi hilo kwa kuwa hukumu yake ilikuwa sawa na kosa la kumlawiti.

## Ashikiliwa na polisi kwa kutishia kuua mtandaoni

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linamshikilia Hamisi Ramadhani kwa kosa la kutishia kuua kwa njia ya mtandao baada ya kumfumania mdogo wake akifanya mapenzi na mke wake.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Mgomi, alithibitisha kukamatwa mtuhumiwa huyo.

Kadhalika katika hali isiyo ya kawaida, watoto wa mtuhumiwa huyo ambao wanasoma sekondari na shule ya msingi wamegoma kuendelea na masomo kwa madai kuwa mama yake amekuwa akimnyanyasa baba yao.

Pia watoto hao wameeleza kuwa hawawezi kuendelea na masomo wakati baba yao akiwa mahabusu.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Danduhu, Kata ya Didia Kwezi Mfaume alisema hayo wakati wa utekelezaji wa mradi wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto unaotekelezwa na Klabu ya Waandishi wa Habari mkoani Shinyanga kupitia Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Mfaume alisema Ramadhani alimshika ugoni mke wake akifanya mapenzi na mdogo wake, kwamba baada ya kumfumania walishindwa kuelewana na kuzuka ugomvi uliosababisha Ramadhani kufikishwa polisi.



Baadhi ya mafundi wa kampuni ya ujenzi wa mradi wa reli ya kisasa (SGR) Yepi Merkezi kutoka Uturuki wakiendelea na ujenzi wa mifumo ya umeme katika kipande cha Isaka-Tabora chenye urefu wa kilometa 165 jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Wananchi wapaza sauti ujenzi holela vituo vya mafuta

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga wameingiwa na hofu baada ya kuibuka wimbi la ajali za moto kutokana na ongezeko la vituo vya mafuta katika makazi yao.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti wananchi hao walisema kitendo cha kujenga vituo vya mafuta jirani na makazi yao kimekuwa ni hatari kwao.

Walisema hali hiyo inatishia usalama wao pamoja na mali zao inapotokea ajali ya moto katika vituo vya mafuta.

Mmoja wa wananchi hao, Joseph Masaga alisema kuna vituo vingi vya mafuta mjini hapo na baadhi vimejengwa jirani na makazi yao.

Alisema serikali inatakiwa kuweka sheria ambazo zitasimamia kuhusu ujenzi wa vituo vya mafuta unaoendelea ikiwamo kuzuia vibali.

Akizungumzia tatizo hilo, Mkaguzi wa Kinga na Tahadhari ya Majanga wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wilayani Kahama, Geofrey Mwita, alisema ujenzi wa vituo vya mafuta kiholela unasababishwa na kutokuwapo kwa ushirikiano kati ya Idara ya Mipango Miji ya Halmashauri pamoja na ofisi yake kwa kuwa wao wamekuwa wakiona ujenzi unaibuka.

"Tulipaswa kushirikishwa kuanzia ngazi ya utoaji wa kiwanja mpaka kuanza kwa ujenzi ili tutoe ushauri, lakini mara nyingi sisi huwa tunaitwa kwenda kukagua jengo ambalo tayari limeshajengwa hali ambayo inakuwa ngumu kumwambia mwekezaji abomoe," alisema Mwita.

Alisema kama wangeshirikishwa kabla ya ujenzi wa vituo hivyo wangetoa ushauri namna ya kuvijenga ili kuepuka madhara inapotokea kimoja kimeungua moto.

Akijibu malalamiko hayo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba, alikiri kuwepo kwa ujenzi holela wa vituo vya mafuta kwenye makazi ya wananchi.

Alisema umbali wa kituo kimoja hadi kingine ni chini ya mita 100 tofauti na maelekezo ya serikali ya umbali wa mita 200 na kuendelea.

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 17, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 13
## Utoro unapotishia kidato cha kwanza, wadau wataja mbinu kuukomesha


Ukurasa 14

MVUA ZINAPOKOLEA
Zitumike kilimo na ufugaji, kupanda miti ya kutosha


Ukurasa 12

Ndivyo ulivyo umuhimu wa kuandikisha elimu ya awali

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

YANAFURAHISHA 2023

# Ni kubadilisha seli kuondoa maradhi, udhaifu

## •Chanjo kuzalishwa 'chap chap', kiufanisi zaidi

MWAKA 2022 unatajwa kuwa ulikuwa wa maendeleo makubwa katika sekta ya sayansi, dawa na safari za anga yote yakiweka msingi wa mafanikio zaidi mwaka 2023.Ni kwa mujibu wa makala ya BBC Swahili yenye kichwa 'mafanikio matano ya kisayansi yanayotarajiwa mwaka 2023'.

Makala inataja kwanza mafanikio kutoka kwa mpango wa Shirika la Anga za Mbali la Marekani (NASA) wa Artemis, ambao ulipeleka mawazo kwenye safari ya mwezini, hadi mbinu mpya za kutengeneza chanjo haraka na kwa ufanisi mkubwa.

Ni katika mwaka wa 2023 pia zinatoka ahadi za kuendeleza maendeleo hayo na kwamba ni mafanikio kadhaa kati ya mengi ambayo yanatarajiwa mwaka huu kubadilisha na kuboresha zaidi maisha ya watu hasa kwenye changamoto za maradhi.

Haya ni baadhi ya mafanikio yaliyo acha alama zisizofutika kwenye sayansi za tiba...



'Uzi wa jeni' ambao una taarifa au tabia ambazo kiumbe huzirithi kutoka kwa wazazi sasa unaweza kupanguliwa, kukatwa na kuboreshwa kukabili maradhi na udhaifu, kupitia utaalamu wa 'gene editing'. **PICHA: BBC**

**MAFANIKIO KICHANJO**

Kipindi kipya cha chanjo kilijiri mwaka jana. Ni hatua kubwa kwa mafanikio ya chanjo za mRNA dhidi ya janga la COVID-19. Aina zote za chanjo zinatengenezwa kwa teknolojia hiyo dhidi ya magonjwa.

Chanjo za kisasa za mRNA hutumia mRNA iliyotengenezwa katika maabara kufundisha seli za binadamu jinsi ya kutengeneza protini au hata kipande cha protini, ambacho huchochea mwitikio na msisimuko wa kinga mwilini.

Mwitikio huo wa kinga, ambao hutoa kinga mwili, ndiyo unaowalinda binadamu dhidi ya kuugua kunakotokana na vimelea au virusi vya jamii hiyo kila vinapotokea sasa na hata baadaye.

Kuna mchanganyiko wa chanjo zinazoundwa zikiwamo za malaria, kifua kikuu, malengelenge yanayojitokeza sehemu za siri, VVU na UKIMWI, 'cystic fibrosis' ambayo ni maradhi yanayoathiri mapafu na mfumo wa chakula, saratani na aina mbalimbali za magonjwa ya mapafu, miongoni mwa mengine mengi.

Kampuni ya kutengeneza dawa ya Ujerumani ya BioNTech inapanga kuanza majaribio ya kwanza ya binadamu ya chanjo yake ya mRNA dhidi ya malaria na kifua kikuu katika muda mfupi ujao, huku kampuni nyingine ya Moderna, ya Marekani, ikifanya hivyo dhidi ya virusi vinavyosababisha madhara na malengelenge sehemu za siri.

Mojawapo ya chanjo zinazotegemewa zaidi ni za mRNA ni dhidi ya saratani. Hizo zimetengenezwa kutambua seli za saratani na kuziharibu ndani ya mwili wa binadamu.

Kampuni nyingine za dawa zinachunguza uwezekano wa kutumia chanjo ya COVID-19 haraka na kwa ufanisi na dawa rahisi ya pua.

Kampuni hizo zimefanya uchunguzi kwenye wanyama na majaribio ya wanadamu yanatarajiwa kufanyika hivi karibuni.

**UKARABATI DNA**

Ni wakati wa kufanikisha ufundi wa kukarabati maumbile CRISPR. Mwaka 2023 unaweza kuwa mwaka ambapo tiba ya CRISPR-Cas9 itaidhinishwa, mbinu ya kuhariri ili kuboresha jeni ambayo inaruhusu uzi wa DNA au nasaba kubadilishwa, kukata sehemu moja na kuiunda upya.

Ni zana au utaalamu wa uhandisi kijeni (genes) inayotumia mfuatano wa CRISPR wa DNA au nasaba na protini inayohusika ili kuhariri jozi au pea msingi za jeni.

Itakumbukwa kuwa DNA au nasaba ni kitu muhimu ndani ya seli ambayo ina taarifa za kijeni zinazohusika na ukuzaji na utendaji kazi wa kiumbe hicho. Kwa mfano kwa binadamu nasaba zinahusika na sura, rangi ya ngozi, kukua, kimo na michakato yote inayorithiwa kutoka kwa wazazi kwenda kwa mtoto.

Matibabu hayo yameonyesha matokeo ya matumaini katika majaribio ya kitiba dhidi ya matatizo mawili ya kijeni au kinasaba kwenye damu, ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa saratani ya damu.

Kampuni za dawa za Vertex na CRISPR Therapeutics zinatengeneza dawa inayojulikana kama exa-cel, ambayo itawasilishwa ili kuidhinishwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Marekani, Machi mwaka huu na ruhusa hiyo itaifanya exa-cel kupatikana kwa wagonjwa walio na saratani ya damu, ulemavu mkubwa wa muundo wa seli nyekundu za damu ambao husababisha mzunguko wa damu wenye matatizo yakiwamo maradhi.

**KUTIBU USAHAULIFU**

Ni maradhi ya Alzheimer ambayo ni matokeo ya seli za ubongo kuharibika na kufa, hatimaye kuharibu kumbukumbu na kazi nyingine muhimu za kiakili zilizo kwenye kukumbuka.

Wakati wowote kuanzia sasa, mdhibiti wa dawa wa Marekani anatarajiwa kutangaza ikiwa dawa hizo zinaweza kupatikana kwa matibabu ya wagonjwa, ingawa dawa hiyo inafaa katika hatua za mwanzo za ugonjwa huo.

Hii ni dawa ya 'lecanemab' ambayo hushambulia ubao wa kunata unaoitwa beta-amyloid ambao hujikusanya katika akili za watu walio na maradhi ya usahaulifu au Alzheimer's.

Katika uwanja wa utafiti huo, dawa hiyo inachukuliwa kuwa mwanzo wa matibabu ya Alzheimer," kwa mujibu wa wataalamu.

Dawa nyingine, inayoitwa 'blarcamesine', ambayo huwezesha protini ambayo inaboresha uthabiti wa nyuroni, itaendelea na majaribio yake ya kimatibabu. Ni tiba inayotengenezwa na kampuni ya dawa ya Anavex Life Sciences.

***BBC***

ELIMU

NA JALIWASON JASSON, BABATI

# Ndivyo ulivyo umuhimu wa kuandikisha elimu ya awali



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mdori wilayani Babati wakimsikiliza Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere (kushoto).
**PICHA: JALIWASON JASSON**

ELIMU ni msingi wa maisha usemi huu unapaswa kutekelezwa kwa vitendo wakati huu wa kuwaandaa wanafunzi wa darasa la awali wanaofikisha wiki ya pili shuleni. Ni muhimu ili kuwajengea nguzo imara kielimu.

Nipashe inazungumza na wazazi na walezi wa watoto wanaoanza elimu ya awali kusikiliza mitazamo yao, katika Kijiji cha Gedamara kilichoko Wilaya ya Babati, Lilian Paschal, anasema amempeleka mtoto wake mwenye miaka minne kupata elimu ya awali ili kuepuka mkono wa sheria na kwamba hataki kusumbuliwa na viongozi wa serikali.

Liliana anasema kuna alikamatwa na mgambo kwa kushindwa kumwandikisha mapema shuleni mtoto.

Mkazi wa Mtaa wa Maisaka A mjini Babati, Faustine John, anasema licha ya serikali kuhamasisha kuandikisha wanafunzi wa darasa la awali mapema wengine hushindwa hadi shule zinapofunguliwa kutokana na kukosa kipato.

Licha ya kwamba elimu ya awali ni muhimu kumwandaa mtoto kujua kusoma, kuandika na kuhesabu, wazazi na walezi inawawia vigumu kuwahi, anasema.

**KUFUATA MWONGOZO**

Serikali imeweka utaratibu wa uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali, Ofisa Elimu Mkoa wa Manyara, Halfani Masukira, anasema.

Anaongeza kuwa uandikishwaji unataka kuanza kuandikisha wanafunzi kuanzia Oktoba hadi Desemba 31 mwaka jana.

Anasema ni kuwaandaa watoto kwenda elimu ya msingi na kila shule inatakiwa iwe na darasa la elimu ya awali na kwamba wanafunzi wa awali vitu vingi anajifunza kwa vitendo zikiwamo picha.

Mtaalamu huyo wa elimu anasema kwa mwaka wa masomo 2022/2023 Mkoa wa Manyara ulikuwa uandikishe wanafunzi wa darasa la awali 46,494 wakiume 23,726 na wa kike 22,768.

Na kwamba hadi kufikia Januari 3 mwaka huu wameandikisha wanafunzi 29,072, wavulana 15,151 wakati wasichana ni 13,921 sawa na asilimia 63 na uandikishaji wa wanafunzi hao unaendelea.

> Mkazi wa Mtaa wa Maisaka A mjini Babati, Faustine John, anasema licha ya serikali kuhamasisha kuandikisha wanafunzi wa darasa la awali mapema wengine hushindwa hadi shule zinapofunguliwa kutokana na kukosa kipato.

Anaeleza kuwa ana imani shule zikifunguliwa idadi itaongezeka mara dufu kwa kuwa wazazi wengi wamezoea kuandikisha wanafunzi siku ya kufungua shule.

Ofisa Elimu anasema sheria ya elimu ya mwaka 1978 inaweza kumchukulia hatua mzazi kuanzia kifungo au faini ambavyo hakutaja ni kiasi gani iwapo hajamwandikisha mtoto shule ya awali.

Mwalimu wa darasa la awali Shule ya Msingi Dudumera, Jemima Njidile, anasema wanafunzi wa awali wakiandikishwa mapema inakuwa rahisi kuanza masomo na wanazoea mazingira na kuwa mahiri zaidi.

Anasema wanafunzi wakiandikishwa mapema inawaondolea usumbufu walimu wa kuanza kurudia mambo ambayo wameishawafundisha wenzao waliotangulia.

Mwalimu wa 'nasari' ya Kituo cha Enhakore kilichoko Babati Mjini Rehema Mwendo, anasema mzazi au mlezi kuwaandikisha wanafunzi wa awali mapema inawasaidia walimu kuwa huru shule zinapofunguliwa na kazi yao inabaki kufundisha na siyo kufanya uandikishaji lakini familia kujua na kuwaandalia mahitaji mapema.

**MAONI YA WADAU**

Mshauri wa awali wa malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto Davis Gisuka kutoka Shirika la Children Incrossfire (CIC) anasema wanafunzi kuandikishwa mapema ni matokeo au sensa inayofanywa na serikali ili kujua umri wa watoto ambao wanastahili kuanza shule na watakaoandikishwa.

Mtaalamu huyo wa malezi na makuzi ya watoto anasema uandikishwaji ukifanyika mapema unasaidia shule kujipanga vizuri namna ya kuwahudumia kwa ufasaha.

Gisuka anafafanua kuwa darasa la awali hakuna masomo ila kuna umahiri kwa mwanafunzi wa kutunza afya, kujua lugha, mazingira na kujifunza kuchangamana na wenzake ili kumfanya ajifunze.

Naye mdau wa elimu wilayani Babati Delfina Reuben, anasema upo umuhimu wa wazazi na walezi kuandikisha watoto wao kuanza darasa la awali mapema ili kuwa na hamasa ya kuanza na kupenda shule.

Delfina anaeleza kuwa uandikishwaji ukifanyika mapema shule inajua mipango yake hasa kujua idadi ya madawati yanayotakiwa kutumiwa wanafunzi wa darasa hilo kufahamu kama wanafunzi wanatakiwa kuwa na mikondo miwili au zaidi na idadi ya walimu, upungufu na kuweka mazingira bora ya kuwafundisha.

Kwa mujibu wa programu jumuishi ya taifa ya malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (PJT-MMMAM) iliyozinduliwa Desemba 2021, Waziri wa Afya (wakati huo) Dk. Dorothy Gwajima, Tanzania ni ya kwanza ukanda wa Afrika Mashariki katika elimu ya awali kuifanya kuwa ya lazima kwenye sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014 ili kujumuisha elimu ya awali kwa watoto wa chini ya miaka mitano.

PJT-MMMAM inaeleza kuwa mtaala wa elimu ya awali unaimarisha ujifunzaji kupitia michezo na mwongozo wa serikali wa mwaka 2016 wa elimu bila malipo hujumuisha elimu ya awali.

Aidha, PJT-MMMAM pia imetoa msisitizo kuwa uandikishwaji wa elimu ya awali ni kiashiria muhimu kilichoingizwa katika mpango wa kitaifa wa maendeleo ya miaka mitano kuanzia 2016/17 hadi 2020/21.

Sera ya elimu ya mwaka 2014 inasema serikali itaweka utaratibu wa elimu ya awali kuwa ya lazima na kutolewa kwa watoto wenye umri kati ya miaka mitatu hadi miaka mitano kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja.

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Utoro unapotishia kidato cha kwanza, wadau wataja mbinu kuukomesha

MATUKIO ya baadhi ya wanafunzi wanaochaguliwa kuingia kidato cha kwanza kutoripoti shuleni kwa wakati, yanaelekea kuwa jambo la kawaida.

Ni kwa sababu yamekuwa yakijirudia kila mwaka katika mikoa mbalimbali, huku sababu kubwa ikitajwa kuwa ni utoro.

Kwa mfano, wanafunzi 4,060 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2022 mkoani Ruvuma, wanaripotiwa kuwa hawajafika shuleni kuanza masomo, sababu mojawapo ikiwa ni utoro, anaeleza Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas.

Utoro huo unasababisha baadhi ya watu kutoa ushauri mbalimbali ambao wanaamini unaweza kusaidia kumaliza tatizo hilo, ambalo kama litaendelea, linaweza kukwamisha maendeleo ya elimu huku serikali ikiigharamiwa kuanzia msingi hadi kidato cha sita.

Miongoni mwa wadau hao ni Sadick Chiguma ambaye katika mazungumzo yake na gazeti hili, anasema ipo haja kwa serikali kufanya utafiti kwa nini baadhi ya wanafunzi hawapendi shule na kutafuta ufumbuzi.

"Inawezekana kuna sehemu haiko sawa ambayo inasababisha baadhi ya wanafunzi wanaochaguliwa kuingia kidato cha kwanza wasiripoti shuleni kwa wakati ndio maana ninashauri serikali ifanye utafiti," anasema.

Anataja taarifa ya Ofisi ya Msemaji Mkuu wa Serikali, kwamba wanafunzi 716, 664 waliotakiwa kuanza kidato cha kwanza, kufikia Januari 15 walikuwa hawajaripoti shuleni akisema inatakiwa kufanyiwa kazi.

"Mimi si mtaalamu wa elimu, lakini kama mzazi, pia mdau wa elimu, hivyo wito wangu ni huo kwamba kwa kuwa matukio ya utoro yanaendelea kujirudia, ni vyema utafiti ufanyike kubaini chanzo cha tatizo na kulikabili," anasema.



Shule zimefunguliwa Januari 9, wanafunzi wahamasishwe kwenda shuleni na kujifunza badala ya utoro. **PICHA: MTANDAO**

### HAKUNA HAMASA

Mdau wa elimu Suzan Lyimo, anasema kinachosababisha baadhi ya wanafunzi kutoripoti shule ni kukosekana kwa hamasa katika elimu, kwa kuwa wapo wanaohitimu bila kujua kusoma na kuandika.

Anasema kwa mazingira kama hayo, wanafunzi wengine wanaona ni bora wakae nyumbani waendelee na shughuli nyingine, badala ya kukazania elimu ambayo wanaona haiwezi kuwaletea maendeleo.

"Hata wazazi na walezi wanakata tamaa, hivyo ni muhimu serikali iboreshe elimu ili kivutia watoto pia. Uboreshaji huo ingeanzia kwenye ujenzi wa mabweni katika sekondari zote za kata," anasema Suzan.

Suzan ambaye kitaaluma ni mwalimu na mwanasiasa, mbunge viti maalum CHADEMA kwa kipindi kirefu, anasema kuwa baadhi ya wanafunzi wa sekondari za kata hutembea umbali mrefu hata kilomita 10 kwenda na kurudi nyumbani, kitendo ambacho kinasababisha wachoke na kuona elimu kama ni mateso kwao.

"Lakini ni muhimu kuboresha mtaala ili kusaidia wanafunzi kuwa na kitu au namna ya kuwawezesha kuendesha maisha yao wanapohitimu, kwani baadhi yao hukata tamaa wanapoona waliohitimu darasa la saba wanafanya shughuli zao wanakuwa na mafanikio lakini wa kidato cha nne hawana mbele wala nyuma," anasema.

Mdau huyo wa elimu, anasema ni muhimu serikali iwekeze kwenye zaidi isaiadie wanafunzi kupiga hatua moja kwenda nyingine badala ya kuhitimu na kujikuta wakiwa mzigo kwa wazazi na walezi.

"Ninaposema kuwekeza kwenye elimu, nina maana kwamba serikali iongeze idadi ya walimu kwani ni wachache lakini idadi ya wanafunzi inazidi kuwa kubwa, hivyo ufundishaji unakuwa mgumu na kusabababisha baadhi ya wanafunzi kutoona umuhimu walimu," anasema.

Anasema baadhi ya watu wanaweza kuchukulia kuwa wiki ya kwanza wanafunzi huwa wanaripoti wachache, baadaye wataongezeka na kwamba hali ya sasa imebadilika, inawezekana wasionekane tena.

### ZIFANYIKE KAMPENI

Godwin Gonde ni Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia Kurasini Dar es Salaam, anasema ili kumaliza tatizo hilo, ni vyema kampeni kubwa ya muda mrefu ifanyike kuhamasisha umuhimu wa elimu.

"Hatua hiyo inaweza kuwafanya wanafunzi, wazazi, walezi na walimu kujali elimu hasa kama mfumo wake utakuwa na manufaa, kwani baadhi yao wamekataa tamaa na mfumo uliopo, kutokana na kwamba wapo waliotimu sekondari na vyuo, lakini hawajaleta mabadiliko chanya kwenye jamii," anasema Gonde.

Anafafanua kuwa jamii haina kitu cha kujifunza kutoka wale waliohitimu, hasa wa wakati huu, na kuongezea kuwa miaka ya zamani aliyesoma alikuwa tofauti na ambaye hajasoma na kwamba ajira zilikuwapo za kutosha na maisha yalibadilika.

"Kwa sasa mtu aliyesoma, hana tofauti na yule ambaye hajasoma, ambaye hajasoma anaweza kufanya mambo makubwa kuliko mwenye elimu ya darasani, hivyo ipo haja ya kuhamasisha umuhimu wa elimu na pia kubadiliko mfumo wa elimu uliopo ambao hamsaidii mwanafunzi kujiajiri," anasema.

Aidha, serikali isitumie nguvu kukamata wazazi au walezi ambao watoto wao hawajaripoti shuleni, badala yake ianzishwe kampeni maalum ya kuhamasisha umuhimu wa elimu, huku mfumo ukibadilishwa, anasema mhadhiri huyo.

"Wadau wa elimu wahusishwe katika kampeni hii ya kuhamasisha jamii kujua umuhimu wa elimu, lakini kikubwa zaidi iwe ni serikali kuangalia mfumo wa elimu uliopo na kuuboresha, ili usisababisha wanafunzi na jamii kwa ujumla kutoona umuhimu wa elimu," anasema.

### HALI ILIVYO 2023

Katika taarifa yake ya Januari 15, mwaka huu kwa vyombo vya habari, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, anasema wanafunzi 716,664 sawa na asilimia 67, wanaotakiwa kuanza kidato cha kwanza mwaka 2023, walikuwa hawajaripoiti shuleni.

Msemaji huyo wa serikali anafafanua kuwa wanafunzi 354,277 kati ya 1,070,941 waliotarajia kuingia kidato cha kwanza sawa na asilimia 33 ya matarajio wakiwamo wenye ulemavu 697, ndio ambao walikuwa wamejiandikisha.

Kutokana na hali hiyo, anatoa wito kwa wazazi na walezi kuhimiza watoto wao waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza waripoti shuleni haraka iwezekanavyo ili waendelee na masomo.

Msigwa akafafanua kuwa serikali inagharimia elimu ya msingi na sekondari kwa kutoa Sh. bilioni 29 kila mwezi na kutoa maelekezo ya kuhusu michango ya wanafunzi wanaoanza shule, ili visiwepo vikwazo vinavyoweza kusababisha wasijiunge na shule.

Aidha, anasema wanafunzi 14,581, wameandikishwa katika Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Waliokosa (MEMKWA), huku 334 kati yao wakiwa ni wale wenye mahitaji maalum.

ELIMU

NA DK. FELICIAN KILAHAMA

MVUA ZINAPOKOLEA

# Zitumike kilimo na ufugaji, kupanda miti ya kutosha

NI vyema kushukuru Mungu, anayetupatia mvua karibu mikoa yote ya Tanzania sasa, ambayo ni muhimu kwa mustakabali wa maisha ya watu na viumbe hai kuanzia mifugo na wanyamapori.

Kwa miezi kadhaa maisha yaligubikwa na tishio la ukame takriban nchi nzima isipokuwa mikoa ya Kanda ya Ziwa Victoria, ambako msimu wa mvua za vuli haukutetereka.

Mikoa mingine ilikuwa na ukame kwa muda mrefu, uliokwamisha upatikanaji wa maji, mito ya Ruaha Mkuu na Ruvu, ikawa haina maji ya kutosheleza kuzalisha umeme kwenye vituo vya Mtera na Kidatu (Ruaha Mkuu) huku maji yakipungua kwa wateja karibu wote.

Kadhalika, ndani ya kipindi hicho gharama za maisha mijini na vijijini zikapanda kutokana na ongezeko la bei za vyakula iliyotokana na mafuta na kusababisha gharama za usafiri na usafirishaji kupaa.

Hata hivyo maeneo yaliyokuwa makavu yanapata mvua na baadhi yakiathiriwa na mafuriko, kuharibika miundombinu ya barabara, madaraja, kuzoa makalvati na kubomoa matuta ya barabara hivyo kusababisha wananchi wakose huduma za usafiri na usafirishaji wa uhakika.

Pamoja na changamoto hizo, Watanzania wanasonga mbele wanaishi na kujitahidi bila kukata tamaa, ili kumudu maisha yao.

Sasa mvua inanyesha watu waitumie na ardhi pia kwa maarifa ili wasisumbuliwe na adui njaa wakati nguvu wanazo, ardhi ipo tena ya kutosha na maji ya mvua hupatikana karibu nchi nzima.

Uzoefu wa miaka mingi, unaonyesha kuwa wengi wanaitumia ardhi kwa kilimo, ufugaji na shughuli nyingine za uzalishaji tena kimazoea bila kuzingatia thamani yake halisi.

Tangu Uhuru 1961 ni kuogelea kwenye kilimo na ufugaji bila kujali athari zake hasi kwa mazingira, matokeo yamesababisha maeneo kadhaa kugeuka jangwa hali ambayo siyo salama kwa mustakabali wa Watanzania.

Kulingana na takwimu za mwaka 2015 za Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa mwaka, Tanzania Bara ilikuwa inapoteza hekta takribani 372,000 za misitu ya asili.



Kupanda miti kulenge matokeo chanya kwa wakulima, wanyama na makazi salama yenye miti na mvua. **PICHA: MTANDAO.**

Mwaka 2017 kituo cha kufuatilia masuala ya 'gesiukaa' (CO2) na athari zake kwa mfumo wa hali ya hewa nchini na duniani cha Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), kilitoa taarifa iliyoonyesha ongezeko la kutoweka misitu Bara kwa kiwango cha hekta 469,000 kwa mwaka.

Hili ni tofauti ya hekta 92,000 zinazoongezeka kila mwaka tangu 2015 na kuashiria uharibifu mkubwa wa mazingira nchini na upotevu wa misitu ya asili.

Kwa kuwa mvua inanyesha katika maeneo mengi nchini, ni vizuri hatua za makusudi na nia njema, zichukuliwe ili rasilimali ardhi itumike vizuri kwa shughuli za kilimo; ufugaji na kuotesha miti ya kutosha.

Katika kutimiza adhma hii ipasavyo, nichukue fursa hii kutahadharisha wakulima walio wengi vijijini; kuachana na 'kilimo cha mazoea'. Kauli hii inamaanisha kuwa: wakulima wamezoea, kwa muda mrefu, wamekuwa na mtazamo kwamba maeneo yenye misitu ya asili ndiyo yanayofaa kwa kilimo. Hivyo, wamekuwa wakifyeka misitu na hatimaye kuchoma moto, kama njia rahisi ya kusafisha shamba au mashamba na kupanda mbegu hususani ni za mazao ya chakula kama mahindi, mtama, ulezi na ngano.



Vilevile, wakulima huotesha mbegu za mazao ya biashara kama pamba, tumbaku, ufuta, kadhalika wafugaji kwa mazoea yao ni 'kuchunga' badala ya 'kufuga'.

Kadhalika, kumekuwapo na mazoea ya kuanzisha makazi mapya vitongoji, katika vijiji vinavyopakana na misitu bila kufuata matumizi bora ya ardhi. Masuala haya yamesababisha kasi kubwa ya kutoweka misitu ya asili.

Ni vyema kuchukua hatua mahususi, kudhibiti matumizi yasiyolenga kuhifadhi mazingira, badala yake kusababisha uharibifu wa ardhi.

Kwanza, halmashauri wilayani ziweke kanuni au sheria ya kuhakikisha kila kijiji kina mpango, uliopitishwa na mamlaka wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji. Kilimo kiwe cha kumwinua mkulima kwa kutumia ardhi ndogo na kuvuna mazao mengi. Kiwe ni kijani kwa misingi ya kuhifadhi udongo lakini kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Maji ya mvua yavunwe na kuhifadhiwa kwa lengo la kufanikisha kilimo endelevu mathalani, wakati wa kiangazi uzalishaji mazao uendelee kupitia fursa za umwagiliaji taifa lineemeke pia kuhifadhi mazingira ipasavyo.

Wataalamu wa kilimo na wengine waliomo katika tarafa au kata mbalimbali; washirikiane na kuhakikisha rasilimali ardhi na maji vinatumika ipasavyo kuwaletea maendeleo endelevu wanavjijiji kwa kutumia rasilimali ardhi vizuri.

Ufugaji pia uwe endelevu na tabia ya kuchunga mifigo kutoka eneo moja kwenda eneo lingine idhibitiwe. Mfugaji awe na sehemu maalumu ya kufugia mifugo yake na kuhakikisha eneo husika analitunza na kuliendeleza ipasavyo.

Isiwe ni kuharibu mazingira ya sehemu fulani halafu kuhamia eneo lingine wakidhani kuwa wao wafugaji wanayo hati-miliki ya maeneo yote Tanzania. Wataalamu wa mifugo wakishirikiana na wenzao katika Tarafa na Kata husika wahakikishe wenye mifugo wanafanya kazi kwa kanuni za tija halisi siyo kuwa chimbuko la migogoro na kuharibu mazingira kwa faida zao binafsi.

Upandaji miti upewe kipaumbele kijamii na kitaifa kwa lengo la kuinusuru Tanzania isigeuke jangwa tukajikuta 'tunaangamizwa kwa kukosa maarifa' wakati maarifa Watanzania tunayo.

Kwa miaka mingi halmashauri nchini zimekuwa na lengo la kupanda na kutunza miti milioni moja na laki tano kwa mwaka.

Hata hivyo hali halisi inaonyesha kuwa lengo hilo halijafanikiwa ipasavyo; kutokana na maeneo mengi nchini kuwa wazi. Sasa ni wakati muafaka kwa Watanzania wote, pamoja na mambo mengine, ni kujikita kwenye kupanda na kutunza miti.

Kwa bahati nzuri watafiti wa Taasisi ya Kufanya Tafiti za Miti (TAFORI) wameainisha maeneo yote na kuonyesha ni aina gani za miti zinazoweza kustawi vizuri katika kila sehemu nchini.

Wataalamu wa misitu, kilimo na mifugo hata wale wa maendeleo ya jamii na mazingira watumie mwongozo huo wa kitaaluma ili matokeo ya zoezi la kupanda miti liwe lenye tija na Tanzania iwe ya kijani.

Kila aliye na uwezo wa kupanda miti apande angalu miti mitatu katika maskani yake. Miwili ya matunda na mwingine wa kivuli mahali pa kupumzikia wakati wa jua kali.

Kama unalo eneo la kutosha tenga sehemu kama eka mbili panda miti inayostawi vizuri katika mazingira hayo kwa faida za baadaye. Licha ya kuboresha hali ya hewa, lakini utavuna miti hiyo itakapokomaa na kupata mbao, nguzo, kuni au mkaa kwa matumizi ya familia au kuuza kupata fedha. Misitu au miti ni rasilimali yenye faida nyingi kwa binadamu:

Ni vyema kupanda miti kwa wingi ili kufaidika siku zijazo. Vilevile, tuhifadhi misitu ya asili iliyobaki kwa manufaa ya leo na vizazi vitakavyofuata.

Wazazi na mababu waliotangulia walihifadhi misitu leo jamii inafaidika kwa kiasi kikubwa; hivyo ni wajibu wa Watanzania wa leo kuhifadhi rasilimali misitu kwa manufaa ya wajukuu wao na vizazi vya baadaye.



## Waganga watakiwa kuweka dawa kwenye vifungashio

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

MKEMIA Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, amewataka waganga na wakunga wa tiba asili kuweka bidhaa zao za dawa ya asili kwenye vifungashio vya kisasa badala ya kuendelea na utamaduni uliopitwa na wakati.

Alieleza hayo jana kwenye mafunzo ya mbinu salama na bora kwa uandaaji wa usindikaji na uchukuaji wa sampuli za dawa asili kwa waganga wa tiba asili na mbadala yaliyofanyika wilayani hapo.

Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na kupitia Umoja wa Waganga na Wakunga wa Tiba Asili Tanzania (UWAWATA).

Mkemia huyo aliwataka kuhakikisha dawa zao zinawekwa kwenye vifungashio vilivyo bora badala ya kuendelea na utamaduni wa kizamani ambao hauna tija na ushindani wa kibiashara.

"Niwaombe waganga na wakunga wa tiba asili boresheni kazi zenu kwa kuifanya kuwa salama zaidi huku wakitengeneza kwenye mazingira yatakayovutia kwa wateja wenu,"alisema.

Aidha, alisema baadhi yao kuna waganga wa tiba asili wanaowaagiza wateja wao wakawabake watoto, bibi na hata wenye ulemavu.

"Wengine wanataka viungo vya watu wenye ualbino ili kufanikiwa hatua ambayo ni ya hatari na huu ni ukiukwaji wa kisheria,"alisema.

Alisema wanapaswa kutumia ujuzi wa dawa zao wanazotumia kwa haki na siyo kwa kuwatapeli na kujifanya wao ni wataalamu wakati ni wachonganishi.

Mkurugenzi Msaidizi Tiba Asili na Tiba Mbadala kutoka Wizara ya Afya, Dk. Paul Mheme, aliwataka waganga na wakunga kujiepusha na uganga wa kimazingaombwe kwa kuwa hauna tija kutokana na sifa walizokuwanazo kwa wateja wao wanaowahudumia.

Alisema kuwa bado kuna waganga wa tiba asili na wakunga ambao wanaojitangaza katika maeneo mbalimbali ikiwamo kwenye miti lakini kazi zao ni za kimazingaombwe na za kitapeli.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Waganga na Wakunga wa Tiba Asili Tanzania, Lucas Mlipo, aliomba ushirikiano kutoka kwa waratibu wa tiba asili na tiba mbadala ngazi ya mikoa, wilaya ili kusajiliwa na kupatiwa leseni za serikali.

Aliomba serikali kupunguza gharama za upimaji wa dawa za tiba kwa mkemia mkuu wa serikali kutokana na sampuli moja inatozwa bei kubwa.

# Watumishi Shirika la Posta watakiwa kutowakwamisha viongozi wao

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MSAJILI wa Hazina, Mgonya Bendicto, amewaasa wafanyakazi wa Shirika la Posta Tanzania kutokwamisha jitihada zinazofanywa na viongozi wao na serikali katika kuhakikisha taifa linafikia azma yake ya uchumi wa kidijitali.

Benedicto alibainisha hayo mwishoni mwa wiki jijini hapo, alipokuwa akifunga Mkutano wa 29 wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa shirika hilo.

"Nafahamu jitihada kubwa zinazofanywa na shirika kupitia viongozi wenu katika kuleta mageuzi ya kulifanya shirika kuwa la kisasa na la kidijitali. Nitumie fursa hii kuwapongeza sana kwa jitihada mnazofanya katika mazingira mliyonayo."

"Kwa sababu hiyo niwaase kila mmoja kwa nafasi yake afanye kazi kwa bidii ili kutokuvunja nguvu juhudi zinazofanywa na viongozi wenu ngazi ya shirika pamoja na viongozi mbalimbali serikalini katika kuhakikisha shirika linakuwa na mazingira wezeshi,"alisema.

Alisema wafanyakazi hao wamefanya jambo jema kupata mafunzo ya uongozi kutoka Taasisi ya Uongozi na kuwataka kuzingatia mafunzo yote kwa kuwa ni muhimu na yana tija kubwa katika nguvu kazi na uzalishaji mali kwa shirika.

Benedicto alifafanua kuwa anafahamu kuwa Baraza la Wafanyakazi ndiyo sehemu muhimu ya kujadili na kupitisha mipango ya maendeleo na bajeti ya shirika na anatambua kikao hicho kimetoa fursa kwa wajumbe kutafakari kwa pamoja wapi shirika limefanya vizuri, vikwazo na mikakati ya kufanya maboresho zaidi.

Postamasta Mkuu wa shirika hilo, Macrice Mbodo, alisema baraza hilo limetoka na maazimio matano ikiwamo kufanya juhudi za kuhakikisha ifikapo Juni 30 mwaka huu, wanapata mzigo mkubwa kutoka kwa wateja waliorudishwa kwa kutoleta mizigo ya kutosha.

Alisema suala lingine ni kufanyika utaratibu wa kukamilisha orodha ya kazi ambayo itaonesha uhitaji wa maofisa masoko mikoani na utaratibu wa kujaza nafasi hizo ufanyike kabla ya 30 Juni, 2023. Aidha, alisema kuwapo mkakati wa kukamilisha usafirishaji wa mifuko kati ya Iringa na Dodoma ufanyike mapema kabla ya Januari 31, 2023 kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji wa mifuko kati ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kati, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Magharibi na Kanda ya Kaskazini.

Pia waliazimia kuwa maeneo ya shirika yaliyobaki pasipo wapangaji yapatiwe wapangaji ifikapo Juni 30, 2023 na kukamilika kwa uwekaji chapa upya katika mikoa yote inayofanyiwa hivyo kabla ya Januari 30, mwaka huu.



Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Fountain Gate Dodoma, Joseph Mjingo (kulia), akipokea funguo za gari la kubebea wagongwa kwa ajili ya matumizi ya shule hiyo lililokabidhiwa na mdau wa elimu na afya, Jacqueline Mmari kwa niaba ya familia ya Makau kwenye hafla iliyofanyika shuleni hapo jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# WB yaridhishwa na TSC inavyotekeleza mradi wa boost

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BENKI ya Dunia (WB) ambayo ni mfadhili wa mradi wa boost imeonesha kuridhishwa na namna Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inavyotekeleza moja ya malengo ya mradi huo katika kuwasaidia walimu kuwa na mwenendo mzuri unaozingatia miiko na maadili ya kazi hiyo.

Mtaalamu wa Elimu kutoka WB ambaye pia ni Msaidizi Mkuu wa mradi wa boost, Gemma Todd, aliyasema hayo kwenye kikao kazi kilichoandaliwa na TSC kwa lengo la kufanya mapitio ya ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu.

Alisema kuwa mradi wa boost unalenga kuimarisha na kuboresha elimu ya awali na msingi kwa shule za serikali ambapo shughuli mbalimbali zimepangwa kufanyika ili kufikia lengo hilo.

Alieleza kuwa katika mazingira ya sasa ambapo kumekuwa na mabadiliko ya kitabia yanayosababisha kuharibika kwa maadili katika jamii ni muhimu kuweka mkazo katika kusaidia walimu kuzingatia miiko na maadili ya kazi yao ili kufanya shuleni kuwa mahali salama kwa wanafunzi.

Alisema kuwa mradi wa boost unatekelezwa na wizara mbili ambazo ni Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) na kueleza kuwa taasisi zilizo chini ya wizara hizo zinazotekeleza mradi huo ni TSC, Taasisi ya Elimu Tanzania, Baraza la Mitihani Tanzania pamoja na Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM).

Mkurugezi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Fatma Muya, alisema kuwa TSC iliandaa andiko la mradi ambalo lilikubalika na kupata ufadhili kufanya mapitio ya ufafanuzi wa kanuni na utendaji kazi katika utumishi wa walimu ambazo walimu wanapaswa kuzitekeleza ili kuboresha elimu na kuwa na shule salama.

Mratibu wa Mradi huo kutoka TSC, Neema Lemunge, alisema pamoja na kazi ya kufanya mapitio ya ufafanuzi wa kanuni za maadili katika utumishi wa walimu, mradi wa boost umefadhili utekelezaji wa shughuli zingine ikiwamo kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazohusu walimu, ununuzi wa vitendea kazi vikiwamo magari na kompyuta.





# Waziri Mkuu atoa onyo kwa wahujumu ruzuku ya mbolea

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewatahadharisha watumishi wa serikali na wananchi wanaoshiriki kuhujumu ruzuku ya mbolea inayotolewa kwa kutorosha kwenda kuuza nchi jirani kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Alitoa tahadhari hiyo jana alipozungumza na wananchi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi akianza ziara ya siku mbili mkoani Mbeya kwa ajili ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema serikali imewekeza Sh. bilioni 150 kwa ajili ya ruzuku hiyo kwa lengo la kuwasaidia wakulima kupunguza gharama ya bidhaa hiyo na kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Waziri Majaliwa alisema fedha hizo zilizotengwa zinatokana na kodi za wananchi wa Tanzania na hivyo kitendo cha baadhi ya watumishi kutorosha na kuuza nchi jirani ni kuwahujumu Watanzania.

Aliwataka wananchi kupinga kwa nguvu zao zote vitendo hivyo ili mbolea hizo zitumiwe ndani ya nchi kama ilivyo makusudi ya serikali ya kuimarisha hali ya chakula.

"Kule Songwe kuna baadhi ya watumishi walikamatwa wakisafirisha zaidi ya tani 2,000 kwenda nchi jirani, hili jambo halikubaliki hata kidogo na mimi keshokutwa naelekea huko tutajua," alisema Majaliwa.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wanazalisha chakula cha kutosha mahitaji ya taifa na ziada inauzwa nje ya nchi ili kujiongezea kipato.

Alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa ya kimkakati kwenye uzalishaji wa chakula na hivyo mbolea nyingi imeelekezwa katika mkoa huo ili kufikia lengo hilo.

Vilevile aliwaagiza mawakala wanaosambaza mbolea kwa wananchi kuhakikisha wanasambaza bidhaa hiyo kwa usawa na kwa wakati katika maeneo yote waliyopangiwa ili wakulima waendane na msimu wa kilimo.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alisema ofisi yake imefanya mazungumzo na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera na kukubaliana kuweka utaratibu ambao utawawezesha mawakala wanaosambaza mbolea kuongeza muda wa kuuza.

Alisema wamekubaliana mawakala hao wauze mbolea hata usiku ili wananchi wote wanaohitaji bidhaa hiyo waipate kwa wakati na kuitumia kwa ajili ya uzalishaji.

Vilevile alisema wameagiza vyama vyote vya ushirika, Bodi ya Mazao Mchanganyiko na Wakala wa Mbolea nchini (TFC) kushirikiana kusambaza mbolea kwa wakulima wa maeneo yote nchini.

"Tumewaelekeza pia mawakala wa usambazaji wa mbolea kuhakikisha wanaongeza vituo vya kuuzia mbolea yakiwamo maeneo ya vijijini ili kuwapunguzia wakulima wa maeneo hayo umbali wa kuifuata bidhaa hiyo huku," alisema Mavunde.

Hivi karibuni Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, alikemea baadhi ya wakulima waliopata mbolea ya ruzuku kuanza kuuza bidhaa hiyo na akawataka kuacha mara moja.

Alisema mbolea hiyo imeletwa na serikali ili kupunguza gharama ya bidhaa hiyo kutoka zaidi ya Sh. 100,000 kwa msimu uliopita mpaka Sh. 70,000 msimu huu.

Vilevile Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alifanya ziara ya kukagua upatikanaji wa bidhaa hiyo katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya na kubaini kuwa baadhi ya mawakala walikuwa wanauza mbolea ya aina moja pekee jambo ambalo lilikuwa linawachanganya wakulima.

Hata hivyo katika Mkoa wa Songwe watumishi saba wa serikali walinaswa hivi karibuni wakiwa wanataka kutorosha zaidi ya tani 2,000 za mbolea kwenda nchi jirani kwa lengo la kuiuza.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua (kushoto), akimkabidhi kishikwambi mmoja wa maofisa elimu kata wa jiji hilo mwishoni mwa wiki, vifaa hivyo zaidi ya 1,000 viligawiwa kwa wakuu wa shule na maofisa elimu kata. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Jeshi la Polisi laanza kampeni upandaji miti ofisini, makazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limeanza kupanda miti katika maeneo mbalimbali ya ofisi na makazi ya maaskari kwa lengo la kutunza mazingira pamoja na kulinda mipaka ya maeneo yake.

Maofisa mbalimbali wa jeshi hilo walishiriki kwenye upandaji wa miti mwishoni mwa wiki kwenye mipaka ya Kambi ya Kikosi cha Kutuliza ghasi (FFU) iliyoko jijini Mbeya.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, alisema katika eneo hilo walipanda zaidi ya miti 420 kuzunguka eneo lote la kambi hiyo.

Alisema lengo la kupanda miti hiyo ni kuunga juhudi za serikali za kutunza mazingira na kulinda mipaka ya maeneo yote yanayomilikiwa na jeshi hilo ili isivamiwe na wananchi na kuzua migogoro isiyokuwa ya lazima.

Kamanda Kuzaga aliwataka maofisa, wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali kuendelea kuilinda na kuitunza miti hiyo ili iweze kukua na kutimiza azma ya utunzaji wa mazingira.

"Tutaendelea na zoezi hili katika maeneo yetu yote na tutahakikisha tunailinda ili ikuwe na itusaidie kwa vivuli, matunda na hasa kulinda mipaka ya maeneo yetu," alisema Kamanda Kuzaga.

Aliwataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya kushiriki pia katika kazi ya kupanda miti katika maeneo yao na ya umma ili kulinda mazingira kama ilivyo nia ya serikali.

Aliwataka pia kupanda miti kwenye vyanzo vya maji ili kuhakikisha vyanzo hivyo vinakuwa endelevu.

# Viongozi wa vijiji wanaogawa maeneo ya uchimbaji kwa rushwa wahadharishwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa vijiji wanaogawa maeneo ya uchimbaji madini katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya kwa kupokea rushwa kwa baadhi ya wachimbaji wametahadharishwa wakitakiwa kuacha tabia hiyo ili kukwepa mkono wa sheria.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, alitoa tahadhari hiyo juzi alipofanya ziara ya kukagua shughuli za uchimbaji katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Mayeka alisema tatizo hilo ni miongoni mwa mambo yanayoifanya sekta ya madini katika wilaya hiyo kushindwa kukua na hata wananchi kutonufaika na madini hayo ambayo ni miongoni mwa rasilimali kubwa katika wilaya hiyo. "Lakini kuna hili tatizo la utoroshaji wa madini, tunaendelea kupambana na tatizo hili kwa kushirikiana na wadau wengine wa sekta hii ili kukomesha tatizo hili," alisema Mayeka.

Aliwataka wachimbaji wa madini kuhakikisha wanauza madini hayo kwenye masoko yaliyoainishwa na serikali ili kuepuka kukumbana na mkono wa sheria.

Alisema mtu yeyote anayekamatwa akitorosha madini hatua ya kwanza serikali inataifisha madini hayo na kumchukulia hatua zingine za kisheria ikiwamo kupelekwa mahakamani.

Alisema kwa sasa kutokana na kukua kwa teknolojia, bei ya dhahabu inakuwa inajulikana katika soko la dunia hivyo wachimbaji wanatakiwa kabla hawajauza dhahabu zao wafuatilie kwanza bei ya soko la dunia. Baadhi ya wachimbaji wa dhahabu waliomba serikali kuwasogezea baadhi ya huduma kwenye maeneo yao ili kuwapunguzia gharama za uendeshaji wa shughuli zao.

Mmoja wa wachimbaji hao, Njunjuru Mhewa, alisema baadhi ya huduma muhimu zikiwamo maabara za kupimia kiwango cha dhahabu zipo Dodoma hali ambayo inawafanya watumie fedha nyingi kwenda kufuata huduma hizo.



## ZAWA yatakiwa kusimamia maeneo ya vyanzo vya maji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, amewataka viongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kuhakikisha wanasimamia suala la uharibifu wa mazingira katika maeneo ya vyanzo vya maji ili kuepusha kutoweka.

Alitoa agizo hilo jana wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi la mradi wa uhuwishaji na uimarishaji wa mfumo wa usambazaji maji Zanzibar.

Alisema serikali haiko tayari kuona mazingira yanaharibiwa kutokana na ukataji wa miti jambo linalosababisha uharibifu wa vyanzo vya maji.

Alisema serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ikiwamo ya majisafi na salama ili kuwaondolea usumbufu wananchi.

"Watendaji wa ZAWA hakikisheni mnawalipa fidia wananchi walioharibiwa mazao yao kutokana na mradi huo lakini pia wananchi kutunza miundombinu hiyo ili iweze kudumu,"alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa ZAWA, Mhandisi Dk. Salha Muhammed Kassim, alisema mradi huo utahusisha matangi mawili, moja litakuwa na ujazo wa lita milioni 2.5, lingine ujazo wa lita milioni nne na utawafikia wananchi zaidi ya 40,000 wa maeneo ya Bweleo, Dimani pamoja na Fumba na utaondoa tatizo la maji katika maeneo hayo.

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Joseph Kilangi, alisema mradi huo ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Aidha, aliwataka wananchi kulinda miundombinu ya maji pamoja na kufuata utaratibu wa uungaji wa maji na kuhakikisha wanachangia ulipaji wa maji ili kuisaidia serikali kupata fedha za kuendesha miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa matangi ya maji.

# Ofisa mradi maliasili ahadharisha athari za mabadiliko ya tabianchi

**Na Rahma Suleiman, aliyekuwa** BAGAMOYO

OFISA mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili, Joseph Olila, amesema mabadiliko ya tabianchi yakizidi kuendelea itasababisha wanyama kuingia katika makazi ya watu kufuata maji au malisho.

Amesema hali hiyo itasababisha migogoro kati ya binadamu na wanyama.

Aliyasema hayo wakati akitoa mada kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa waandishi wa habari kuhusu uhifadhi na mazingira yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) yaliofanyika wilayani Bagamoyo mwishoni mwa wiki.

Olila alisema pia kuna hatari kubwa ya kupoteza bayoanuai iliyoko kwa sababu mabadiliko ya tabianchi yanapozidi yatasababisha wanyama kupotea na watashindwa kuhimili mabadiliko hayo.

Alisema athari hizo za mabadiliko ya tabianchi yanaweza kusaabisha matatizo kwenye jamii kwa sababu mwingiliano kati ya binadmau na wanyama unazidi kuwa hasi na wanyama kusogea katika maeneo ya binadamu kwa kufuata malisho na maji.

Alisema hali hiyo kama haijadhibitiwa itasababisha wanyama kuathirika na kuathiri jamii na jamii inavyoathirika inazidi kuwa masikini na kupunguza uwezo wao wa kuhimili mabadiliko hayo.

Aidha, alisema wapo baadhi ya wanyama hawawezi kuhimili mabadiliko ya tabianchi mfano viumbe vidogo ambavyo haviwezi kuhimili joto ikiwamo vyura au vinyonga ambao uwezo wao ni mdogo kuhimili hali hiyo.

"Kinyonga hawezi kutoka eneo moja kutembea kilomita 60, mazingira mazuri ya kuishi hivyo likitokea tatizo katika eneo lake yupo katika hatari za kuhimili matatizo kwenda kutafuta chakula," alisema.

Alisema ili kuondokana na changamoto hizo kuna baadhi ya mikakati muhimu kama taifa kuifanya ikiwamo mipango mizuri ya matumizi ya ardhi ili kuwapo kwa maeneo ya kuruhusu wanyama wapite kutoka eneo moja kwenda jingine.

Alisema lazima taifa kuwa na miakakti ya kusaidia viumbe hai ambao wapo hatarini ili kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kwenye mfumo wa kiikolojia hakuna mnyama asiye na umuhimu na kila mnyama anapopotea kwenye mfumo huo kuna huduma hupungua hivyo kuzidi kuvipoteza viumbe jamii itakosa huduma muhimu ikiwamo chakula.

Olila alitolea mfano wa nyuki ambaye ni kiumbe mdogo lakini anafaida kubwa kwenye uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na ikitokea kuwapoteza athari pia kuzalisha mimea inapungua hivyo ni muhimu kuhakikisha viumbe wote hawapotei.

Alisema kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi wanyama hutembea na hutoka kwenye maeneo ya hifadhi kutafuta malisho na maji ambayo inahatarisha maisha yao na majangiri ni rahisi kuwakamata au kuwaua.

Alisema lazima kuweka kipaumbele katika uhifadhi kwa sababu unamchango mkubwa katika uchumi na jamii hivyo kuweka rasilimali za kutosha katika kupambana na ujangiri na maeneo ya uhifadhi yanasimamiwa vizuri ili kutowapoteza viumbe hai na kufaidika na uhifadhi.

Mkurugenzi wa JET, John Chikomo, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo waandishi wa habari kuripoti masuala ya uhifadhi na mazingira ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema waandishi wa habari watakapopaza sauti zao kupitia taaluma yao wananchi watafahamu umuhimu wa kuhifadhi mazingira na maliasili ambapo miongoni mwa athari za mabadiliko ya tabianchi yanasababishwa na binadamu.

"Uharibifu wa mazingira ikiwamo ukataji wa miti ni miongoni mwa uwapo wa athari za mabadiliko ya tabianchi katika jamii yetu," alisema.

Waandishi wa habari 25 kutoka vyombo vya habari Tanzania Bara na Visiwani walisema bado jamii inahitaji kupewa elimu kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira na kulinda maliasili ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.



Waziri wa Mambo ya Ndani ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Kikwajuni, Mhandisi Hamad Masauni, akisalimiana na Mzee Idd Abdala Seif jimboni kwake, Unguja, Zanzibar alipokuwa kwenye ziara ya kutembelea wazee na wagonjwa jimboni humo jana. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NDANI**

# Jamii yakumbushwa umuhimu wa kudai haki za msingi

**Na Mwandishi Wetu**

JAMII imetakiwa kutambua umuhimu wa kudai haki zao za msingi ili kuimarisha ustawi wa jamii na usawa katika maendeleo ya nchi na watu wake.

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Tathmini na Ufuatiliaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, Zanzibar (TAMWA ZNZ), Mohamed Khatib, katika mkutano wa kamati za wananchi wa Shehia za Wilaya za Micheweni, Wete, Mkoani na Chake Chake Pemba ulioandaliwa na Jumuiya ya Utetezi wa Mazingira na Jinsia Pemba (PEGAO), kwa kushirikiana na TAMWA ZNZ.

Alisema lengo la kuzijengea uwezo kamati hizo ni kufuatilia kero zinazokwaza haki za wanawake zilizoibuliwa na wahamasishaji jamii kwenye maeneo yao na kuhimiza jamii kuendeleza utamaduni wa kukutana kujadili kero zinazowakabili ili kuzitafutia suluhu kwa pamoja.

"Lazima kamati hizi zikutane na wananchi ili wao wenyewe waseme wana tatizo gani kuliko kuwasemea, hii itasaidia kuwa na uthibitisho na ushahidi wa kutosha juu ya matatizo yoyote inayotafutiwa ufumbuzi," alisema.

Alisema kuwa kupitia ushirikishwaji wa wananchi kujadili matatizo na kero zinazowakabili wanawake kupata haki zao, itasaidia kukuza uelewa wa jamii kushiriki moja kwa moja na kudai haki hizo zikiwamo za upatikanaji wa huduma muhimu za jamii.

Aidha, aliupongeza Ubalozi wa Norway kwa kushirikiana na TAMWA, Jumuiya ya Wanasheria Wanawake (ZAFELA) na PEGAO kutekeleza mradi huo unaolenga kujenga jamii yenye uwezo wa kupaza sauti kwenye kero zinazowakosesha wanawake haki za msingi katika jamii.

Mkurugenzi wa mradi huo kwa upande wa PEGAO, Hafidh Abdi, alisema jamii inapaswa kutambua kwamba ina wajibu wa kukabiliana na matatizo yanayowakabili ili kujenga jamii yenye kufuata misingi ya usawa wa kijinsia kwa wote katika kila eneo.

"Wananchi wanatakiwa wajue kwamba kero zilizoko katika jamii ni zao na wanao wajibu wa kuzitafutia ufumbuzi kwa njia sahihi ili kuwapo na misingi ya upatikanaji wa haki za msingi kwa kila mmoja hasa wanawake katika nyanja zote ikiwamo kiuongozi," alisema Hafidh.

Mratibu wa TAMWA kutoka Pemba, Fat-hiya Mussa, aliwataka washiriki wa mkutano huo kuihamasisha jamii kupaza sauti za kudai haki zao zikiwamo za kijamii badala ya kuzisubiri kupatiwa na serikali na vyombo vyake.

"Ni lazima wananchi wawe na uelewa wa kutosha juu ya zipi ni haki zao na namna gani wanapaswa kuzidai kwa njia iliyo sahihi ili kuondoa matatizo zinazoikabili jamii ikiwamo ya uhalifu," alisema.

Mmoja wa wajumbe wa kamati hizo, Mohamed Abdalla alihimiza jamii kutumia vyombo vya habari kupaza sauti zao ili matatizo yanayowakabili ziweze kuwafikia walengwa kwa wakati.

Kamati za wananchi katika shehia zilizoundwa kupitia mradi huo unaofadhiliwa na Ubalozi wa Norway, zinafanya kazi kwa kuwashirikisha wananchi kujadili matatizo na vikwazo vinavyowakabili hasa wanawake na kupelekea kushindwa kupata haki zao za msingi ikiwamo ushiriki wao katika uongozi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LEOPORD PHILEMON MLOWE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **MITSUBISH CANTER** yenye usajili namba **T 827 DPM, CHASSIS NAMBA: FE648E520379** na **ENGINE NAMBA: 4D35D98733.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: NJ/TR/RB/109/2023**

---

**SUBSTITUTION SUMMONS**
**IN THE DISTRICT COURT OF BUKOBA AT BUKOBA**
**APPLICATION FOR EXECUTION NO.8/2023**
**[Originating from Civil Case NO. 05/2021 Of the District Court of Bukoba]**
**GESAP ENGINEERING GROUP LTD......DECREE HOLDER**
**VERSUS**
**SONIA ENTERPRISES COMPANY LIMITED.......1ST J/DEBTOR**
**MAHAMUD HAJI SWAHIBU.........2ND J/DEBTOR**

**NOTICE OF MENTION**

TO:MAHAMUD HAJI SWAHIBU
TAKE NOTICE that the mention case has been set down for Hearing On the 27THday,2023 of JANUARY at 8;30 O'clock in the forenoon, Before Hon.A.W.KABUKA -RM. Your presence is therefore required on the date and the time indicated.
Given under my hand and the seal of the court this 6th day of JANUARY,2023

RESIDENT MAGISTRATE
BUKOBA

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**ABUBAKAR K. HUSSEIN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3861-0046** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya ANDERLEK RIDGES mwaka 2015, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **TAB/RB/180/2023**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**THABITI SOUD MGONANZE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA LITEACE PICK-UP** yenye usajili namba **T 752 DGY , CHASSIS NAMBA: KM510067899** na **ENGINE NAMBA: 5K452541GY.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DSM/PHQ/RB/498038/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JAZMAK MOTORS LTD** anatangaza kupotea kwa kadi Ya gari aina ya **VEROSA yenye** usajili namba **T890 CLB, CHASSIS NAMBA: GX1106051559** na **ENGINE NAMBA: 1G5947851 .** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/KIL/RB/494933/2022**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 02 OF 2023**
**In the Matter of the Estate of the Late:**
**JOYCE JOHN MLENGE**

**By 1. INNOCENT CASSIAN MLENGE**
**2. .......................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the **23 day of JANUARY..2023**
Dated at Morogoro this **10 day of JAN..2023**

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**TULIZA JACOB SANGA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI AINA YA TVS KING YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.580 BNL.**YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI
**MBE/MBE/RB/21288/2023**

---

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na Mahakama Kuu Iringa, tutauza kwa mnada wa hadhara mali za wadaiwa kama ifuatavyo:

**TALAKA No 30/2022**

MDAI...................HUSNA H. KONDO
MDAIWA............GEORGE NYAGAWA

Nyumba iliyopo DON BOSCO KISIWANI – IRINGA MJINI itauzwa tarehe 23.02.2023 na mnada utafanyika saa tano(5:00) asubuhi.

Masharti yaliyoandikwa kwenye mbao yazingatiwe.

**Kwa mawasiliano zaidi:**
**0655 136010 AU**
**0748 237245**

**MAJEMBE AUCTION MART LTD-IRINGA**

---

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# NATO yaahidi kuipatia Ukraine silaha zaidi

**KYIV, Ukraine**

KATIBU Mkuu wa Jumuiya ya Kujihami ya NATO Jens Stoltenberg amesema Ukraine itarajie kupata silaha nzito zaidi hivi karibuni ambazo zitawasaidia kuimarisha ulinzi na kukabiliana na mashambulizi ya Russia.

NATO iliahidi kuipa Ukraine silaha nzito zaidi jana, baada ya zaidi ya watu 30 kuuawa Ukraine kutokana na mashambulizi ya Russia, huku Rais Vladimir Putin akivipongeza vikosi vyake vilivyodai kuukamata mji wa Soledar.

Huku idadi ya vifo ikipindukia 30 na shughuli za kufukua vifusi na kutafuta makumi ya watu ambao bado hawajulikani waliko ikiendelea baada ya Russia kushambulia kwa kombora jengo la ghorofa la makazi ya watu juzi, katibu wa NATO Stoltenberg alisema Ukraine itarajie silaha nzito kutoka kwa washirika wake.

Aidha, inaelezwa kuwa ahadi hiyo inatokana na ombi la Ukraine kwa washirika wake kuipa vifaru, makombora na zana zaidi ambazo ni muhimu katika kujilinda.

Katika kuelekea mkutano unaotarajiwa kufanyika wiki hii, wa kundi linaloratibu shughuli za usambazaji silaha kwa Ukraine, Stoltenberg ameliambia jarida la kila siku la Ujerumani Handesblatt kwamba ahadi za kuipa Ukraine zana nzito ni muhimu na anatarajia ahadi zaidi zitatolewa siku zijazo.

Hata hivyo shambulizi hilo la Russia limelaaniwa vikali na Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky.

"Kwa sasa hatima ya zaidi ya watu 30 ambao huenda walikuwa kwenye jengo hilo lililoko Dnipro wakati kombora la magaidi liliposhambulia haijulikani, makumi ya watu waliokolewa, wakiwamo watoto sita, tunapambana kumpata kila mtu," alisema Zelensky.

Rais Zelensky aliziomba nchi za magharibi silaha zenye nguvu zaidi, akisema ugaidi wa Russia unaweza kukomeshwa tu katika uwanja wa mapambano.

Mapema mwezi huu, Ufaransa, Ujerumani na Uingereza ziliahidi kuipa Ukraine, vifaru magari maalum ya kivita miongoni mwa silaha nyingine.

Vile vile inaelezwa kuwa kuna ongezeko la shinikizo kwa washirika wa Ukraine kupiga hatua zaidi na wakubaliane kuipa Ukraine silaha zenye nguvu na ubora zaidi.

Naye Waziri Mkuu wa Uingereza, Rishi Sunak, mwishoni mwa juma lililopita aliahidi kuipa Ukraine vifaru 14 aina ya Challenger 2.

Ubalozi wa Russia nchini Uingereza ulitahadharisha kuwa kupeleka vifaru hivyo katika uwanja wa mapambano, kutachochea mashambulizi zaidi na maafa mengi hata kwa raia.

*DW*



Mtaalamu wa afya akimpatia mtoto matone ya chanjo ya polio ikiwa ni kampeni iliyozinduliwa juzi nchini Pakistan, ikilenga watoto milioni 44.2 walio chini ya umri wa miaka mitano. **PICHA: AP**

# Museveni ataka marufuku ya kusafiri kwa wabunge

**KAMPALA, Uganda**

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, ametoa wito wa kupiga marufuku safari za nje ya nchi kwa wabunge na watumishi wa umma ili kuokoa fedha kwa mambo mengine yenye kipaumbele zaidi.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita alipokuwa akituma vifaa katika Taasisi ya Petroli ya Uganda Kigumba (UPIK), eneo ambalo nchi hiyo inatarajia kutoa mafunzo kwa wataalamu wa ndani katika utafiti wa mafuta.

Uganda inatarajia kuanza kusukuma mamilioni ya mapipa ya mafuta ifikapo mwaka 2025 kutoka kwenye hifadhi yake kubwa ya mafuta, lakini Rais hakufurahishwa na kwamba taasisi ya mafunzo bado haijakamilika kutokana na ukosefu wa fedha.

Kwa mujibu wa taarifa ya vyombo vya nchini Uganda, Rais Museveni alisema; "Waambie watumishi wa umma na wabunge waache kusafiri nje ya nchi. Pesa zinapotea katika safari za nje na bado Kigumba inalilia pesa."

Rais huyo pia alipendekeza kusimamishwa kwa posho zote, kwa mujibu wa tovuti ya habari ya Daily Monitor.

Aidha, bomba la mafuta ghafi linalogharimu dola bilioni 3.5 litakalounganisha maeneo ya mafuta ya Uganda mpaka Bandari ya Tanzania limepingwa na wanaharakati wa hali ya hewa. Licha ya kwamba nchi hizo mbili za Afrika Mashariki zinasema kipaumbele chao ni maendeleo ya kiuchumi.

*BBC*

## Mkenya akamatwa kuhusika na mauaji DRC

**KINSHASA, DRC**

RAIA wa Kenya amekamatwa kwa kuhusishwa na shambulio la mlipuko wa bomu kwenye kanisa moja huko Kasindi katika Jimbo la Nord Kivu Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Msemaji wa jeshi la kanda ya DRC Kapteni Anthony Mualushayi, alisema mshukiwa alikamatwa katika kituo cha mpakani cha Kasindi muda mfupi baada ya shambulio hilo.

Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Felix Tshisekedi, alilaani vikali shambulio hilo na kuahidi kuwafikisha wahalifu mbele ya sheria.

Inabainishwa kuwa takribani watu 17 wamefariki dunia na wengine zaidi ya 30 kujeruhiwa kutokana na mlipuko wa bomu hapo uliotokea juzi mchana wakati wa ibada huko Lubiriha katika wilaya ya Beni mashariki mwa DRC.

Inaelezwa kuwa waasi wa ADF wanaendelea kuwa tishio kwa usalama wa raia wanaoishi mashariki mwa DRC.

*BBC*

## Tatizo la nishati laendelea kuitikisa SA

**CAPE TOWN, Afrika Kusini**

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, amesitisha mipango wa kuhudhuria kongamano la kiuchumi duniani mjini Davos Uswizi kwa sababu ya mzozo wa nishati unaoendelea kuiathiri nchi yake.

Hiyo ni kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na msemaji wa Rais huyo Vincent Magwenya na kwamba Afrika Kusini inakumbwa na hali isiyo ya kawaida ya kukatika kwa umeme katika kipindi cha miezi 12 iliyopita kutokana na matatizo ya kampuni ya serikali ya umeme ya Eskom.

Magwenya alisema Ramaphosa alikuwa anatarajiwa kuongoza ujumbe wa serikali kwenye mkutano huo mkubwa wa kiuchumi katika milima ya Uswizi wiki hii lakini badala yake atabaki nyumbani kufanya mazungumzo na Eskom na viongozi wa kisiasa.

"Kutokana na tatizo la nishati linaloendelea Rais Ramaphosa amesitisha ziara yake ya kwenda kushiriki katika kongamano la kiuchumi la dunia huko Davos," alisema na kuongeza:

"Kwa sasa Rais ameitisha kikao na viongozi wa vyama vya siasa vyenye uwakilishi bungeni, kamati ya kitaifa ya mzozo wa nishati (NECCOM) na Bodi ya Eskom." alisema.

*VOA*

# GGML YAONGEZA UDHAMINI WA MAMILIONI GEITA GOLD FC

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML), imeongeza mkataba wa udhamini kwa Klabu ya Geita Gold (GGFC), wenye thamani ya Sh. milioni 800 kuanzia ambao umeanza rasmi jana.

GGML ilipata haki ya kipekee kama wadhamini wakuu wa klabu hiyo kwa mechi na matukio yote yanayohusiana na Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022-2023 (NBC Premier League).

Katika msimu wa 2020/21, Klabu ya Geita Gold ilitimiza malengo kadhaa ikiwa ni pamoja na kushiriki katika mechi za kimataifa jambo ambalo limeonyesha thamani ya udhamini walikuwa wamepewa.

Geita Gold, iliyokuwa ikishiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, ilipata mafanikio hayo kwa mara ya kwanza baada ya kushika nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu ya NBC msimu uliopita.

Katika hafla ya utiaji saini iliyofanyika hivi karibuni kwenye Makao Makuu ya Halmashauri ya Mji wa Geita, Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Terry Strong, alisema makubaliano hayo yameifanya kampuni hiyo kuwa wadhamini wakuu wa Klabu ya Geita Gold.

"Msimu uliopita, GGML ilikubali kudhamini Geita Gold Football Club kwa Sh. milioni 500, hata hivyo udhamini wetu sasa umeongezwa hadi Sh. milioni 800.

"Kama ilivyotajwa kwenye MOU (mkataba wa makubaliano), GGML ingependelea udhamini huu kuwezesha ununuzi wa basi la klabu, huduma ya chakula kwa timu na vifaa vya michezo. Tunatarajia udhamini wetu utarahisisha ushiriki wa timu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022-2023, pamoja na shughuli nyingine za klabu," alisema Strong.

Mkuu wa Wilaya ya Geita, Wilson Shimo, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo ya utiaji saini alifurahishwa kuona pande hizo mbili zikitia saini makubaliano hayo kwa kuwa yatakuwa na ushawishi chanya mkoani Geita.

"Geita Gold Football Club ni kielelezo cha sifa chanya za Mkoa wa Geita. Timu imefanikiwa kutambulisha wilaya na mkoa wetu. Kwa sasa kila mtu anafahamu eneo la kijiografia ya mkoa wetu," alisema na kuzitaka pande hizo mbili kufikiria kujenga chuo cha michezo mkoani Geita ili kuibua vipaji vya vijana.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Zahara Michuzi, naye aliipongeza GGML kwa kuwa na moyo wa kujitolea kwa ajili ya Klabu ya Geita Gold.

"Ufadhili huu wa GGML katika klabu hii umekuwa na matokeo chanya. Shauku na juhudi za wachezaji ni matokeo ya uwekezaji wa GGML. Tunashukuru kwa dhati kutokana na msaada huu," alisema.




Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Terry Strong (kulia) na Makamu Mwenyekiti wa Geita Gold FC, Pole Zengo, wakionyesha mkataba wa udhamini uliosainiwa kati ya pande hizo mbili. Waliokaa kutoka kushoto ni Mbunge wa Geita, Constantine Kanyasu (CCM), Mkuu wa Wilaya ya Geita, Wilson Shimo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Zahara Michuzi na Kaimu Meneja Mwandamizi wa Masuala ya Jamii wa GGML, Moses Rusasa. **MPIGAPICHA WETU**

# Mandonga ulingoni tena 'Usiku wa Kisusio'

**Na Saada Akida**

BONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, Ismail Galiatano, anatarajia kupanda ulingoni dhidi ya Asanda Gingqi raia wa Afrika Kusini katika pambano la Kili Boxing Tours litakalofanyika Februari 25, mwaka huu mkoani Kilimanjaro huku wakisindikizwa na mwanamasumbwi mwenye maneno na mbwembwe nyingi, Karim Mandonga, imeelezwa.

Mandonga ambaye kwa sasa anatamba na ngumi yake anayoita 'Sugunyo', akijinasibu imetoka Ukraine kwenye mlipuko wa mabomu, atapanda ulingoni akitoka kushinda wiki iliyopita ugenini nchini Kenya kwa TKO dhidi ya Daniel Wanyonyi.

Pambano hilo la Februari 25, ambalo limepewa jina la 'Usiku wa Kisusio' limepangwa kupigwa katika Ukumbi wa YMCA ulioko Moshi mkoani Kilimanjaro.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na waandaji wa pambano hilo, Kampuni ya Peak Time Media chini ya Promota, Meja Selemani Sumunyu, imeeleza kuwa katika pambano hilo la Galiatano na Gingqi, pia bondia mwenye maneno na mbwebwe nyingi, Mandonga, anatarajiwa kupanda ulingoni.

Taarifa hiyo imewataja mabondia wengine wengi watakaopanda ulingoni usiku huo huku ikieleza kuwa bondia atakayepambana na Mandonga bado hajawekwa wazi pamoja na mpinzani wa mwanadada, Batuli Yassin.

Lakini ikaeleza kuwa bondia mkali na mwenye uzoefu wa kutosha Ramadhani Shauri atapanda ulingoni dhidi ya Mwinyi Mzengela wakati Alibaba Tarimo akitarajia kucheza na Salim Abeid.

Wengine watakaopanda ulingoni kwenye pambano hilo ni Mohamed Pesa ambaye atacheza na Iman Bariki huku Hussein Itaba akipewa Joseph Maigwisa na Shaban Ndaro akitarajiwa kuvaana na Musa Dragon wakati Kassim Hamad akifungua dimba na Gabriel Chola.

# KMKM kutetea ubingwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya KMKM SC imesema licha ya juzi kupata ushindi mnono wa mabao 3-0 dhidi ya Kundemba FC katika mchezo wao wa raundi ya 16, bado wanahitaji kupambana ili kuhakikisha wanatetea taji lao la ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Ame Msimu, alisema katika mzunguko huu wa pili timu hiyo imejipanga kuhakikisha inafanya vizuri zaidi kwa kupata alama kwenye kila mchezo ili lengo lao litimie.

Alisema anajua mzunguko huu timu zote zimejiimarisha kwa kusajili wachezaji wa kuimarisha vikosi vyao kwenye dirisha dogo kulingana na timu zao, lakini na wao wamejipanga kukabiliana na mapambano yote hasa ya mbio za ubingwa.

Alisema katika mchezo wao juzi dhidi ya Kundemba FC, wameona viwango vya wachezaji wao vimeimarika na wanacheza kwa mujibu wa maelekezo ya mwalimu licha ya wapinzani wao kuonyesha ushindani hasa kipindi cha pili.

"Timu yetu imecheza vizuri sana kwa kufuata mfumo wa mwalimu, licha ya mapungufu madomadogo kwa safu ya ulinzi ambayo yataweza kumalizika katika mchezo ujao, sasa hivi tumeingia katika mzunguko wa mapambano wachezaji wanatakiwa kujua nini hasa lengo letu," alisema.

Timu ya KMKM imefikisha alama 32 ikitinga nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar wakati Kundemba FC ikiendelea kusalia nafasi ya 12 ikiwa na pointi 16.

Ligi Kuu Zanzibar itaendelea tena leo Jumanne kwa kuikutanisha timu ya Mlandege FC dhidi ya Chipukizi mchezo utakaochezwa katika Uwanja wa Amaan majira ya saa moja za usiku.

## ZISIKUPITE

### STERLING SASA KUUZWA

CHELSEA iko tayari kusikiliza ofa kwa mshambuliaji wa England, Raheem Sterling, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, kuhamia Stamford Bridge msimu uliopita wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### RAPHINHA AWANIWA ARSENAL

KLABU ya Arsenal imewasiliana na Barcelona ili kumnunua winga wa Brazil, Raphinha, mwenye umri wa miaka 26. ***(90min)***

### BARCA YATANGAZA BEI

BARCELONA imeweka bei ya euro milioni 100 kwa Raphinha, ambaye alihamia Nou Camp kutoka Leeds United Julai mwaka jana. ***(Sport)***

### AUBAMEYANG ATAKIWA BARCA

BARCELONA inataka kumsajili tena fowadi wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, mwenye umri wa miaka 33 kutoka Chelsea. ***(Telegraph)***

### CHELSEA NA PAUNI MIL. 100

CHELSEA iko tayari kutumia zaidi ya pauni milioni 100 kununua wachezaji wengine watatu katika dirisha la uhamisho la Januari baada ya kukamilisha dili la kumnunua fowadi wa Ukraine, Mykhailo Mudryk. ***(Football Insider)***

### FRESNEDA AWANIWA ARSENAL

KLABU ya Arsenal ina nia ya kumsajili beki wa kulia wa Real Valladolid, Ivan Fresneda, mwenye umri wa miaka 18. ***(Telegraph)***

### GERRARD ANUKIA POLAND

MAJADILIANO yanaendelea kati ya Chama cha Soka cha Poland na Steven Gerrard kuhusu kuchukua nafasi ya kuwa kocha mpya wa timu ya taifa. ***(Fabrizio Romano)***

### HENRIQUE AGOMBEWA EPL

KLABU ya Manchester United na Arsenal itashindana kumsajili winga wa Brazil, Luiz Henrique, 22, kutoka Real Betis. ***(Fichajes)***

### MOFFI KWA WEST HAM

KLABU ya West Ham imetoa ofa ya pauni milioni 25 kumnunua mshambuliaji wa Lorient na Nigeria, Terem Moffi mwenye umri wa miaka 23. ***(Sky Sports)***

### LAMMENS ANYATIWA LEEDS

LEEDS United inavutiwa na mlinda mlango wa Club Bruges raia wa Ubelgiji, Senne Lammens, mwenye umri wa miaka 20. ***(Mirror)***

### CANTWELL ATAJWA PSV

PSV Eindhoven inamtaka kiungo wa kati wa Norwich, Todd Cantwell mwenye umri wa miaka 24. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AANZA KUOTA UBINGWA EPL ARSENAL

●●●Tukifanya kazi yetu tunafurahisha watu wengi na nina uhakika tumewafurahisha sana mashabiki wetu, hivyo...

**LONDON, England**

MIKEL Arteta anahisi Arsenal "imepiga hatua nyingine" baada ya ushindi muhimu wa 'dabi' dhidi ya Tottenham Hotspur uliowafanya kuwa pointi nane zaidi kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England dhidi ya Manchester City inayoshika nafasi ya pili ikiwa na alama 39.

Hugo Lloris alijifunga kabla ya Martin Odegaard kuongeza la pili huku utawala wa Arsenal katika kipindi cha kwanza ukiwapa ushindi wa mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur, Jumapili.

Hilo liliwaacha Arsenal wakiwa na uongozi wa pointi nane kileleni mwa Ligi Kuu ya England na Arteta anaamini kuwa timu yake ilidhihirisha kuwa inawania taji.

Arteta aliiambia Sky Sports: "Nilipenda jinsi tulivyocheza na ujasiri tulioonyesha kuja hapa na kucheza.

"Tukifanya kazi yetu tunaweza kuwafurahisha watu wengi na nina uhakika tumewafurahisha sana mashabiki wa Arsenal. Kila kitu tunachouliza, wako tayari kujaribu kufanya.

"Ni kundi la wachezaji wa kutisha, nadhani leo (juzi), tumepiga hatua nyingine, tulishinda msimu uliopita kwenye viwanja vikubwa, lakini jinsi tulivyoshinda ilikuwa ya kupendeza kutazama.

"Inaonyesha si tu dhamira na ujasiri, lakini lazima uwe na imani na ubora wa kufanya hivyo dhidi ya timu hii. Hilo linategemea kabisa wachezaji.

"Tulikuwa wakali sana. Tulikuwa wakali sana dhidi ya wachezaji wa hali ya juu. Tulishinda mipira mingi na pambano. Walitengeneza nafasi kadhaa, ni timu hatari, lakini tulifanya kazi nzuri."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,067,6

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 18,19 NA 20 JANUARI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/01/23 | 18:00 | Talaea El Gaish vs Ismaily SC | 2.83 | 2.68 | 2.88 |
| 02. 18/01/23 | 19:00 | DR Congo vs Ivory Coast | 3.44 | 3.04 | 2.22 |
| 03. 18/01/23 | 22:00 | AC Milan vs Inter | 2.85 | 3.34 | 2.44 |
| 04. 18/01/23 | 22:45 | Livingston vs Dundee Utd | 2.43 | 3.23 | 2.83 |
| 05. 19/01/23 | 17:30 | Gaziantep BB vs Konyaspor | 2.53 | 3.22 | 2.53 |
| 06. 19/01/23 | 18:00 | National Bank vs El Ittihad Alexandria | 2.31 | 2.84 | 3.44 |
| 07. 19/01/23 | 23:00 | Villarreal vs Real Madrid | 3.03 | 3.43 | 2.21 |
| 08. 20/01/23 | 14:00 | Gokulam Kerala FC vs Real Kashmir | 2.25 | 2.98 | 3.12 |
| 09. 20/01/23 | 19:00 | Istra vs Slaven Belupo | 2.31 | 3.10 | 2.91 |
| 10. 20/01/23 | 20:30 | Sochaux vs Caen | 2.33 | 3.12 | 3.02 |
| 11. 20/01/23 | 21:30 | Cholet vs FC Martigues | 2.87 | 3.16 | 2.38 |
| 12. 20/01/23 | 21:30 | Saint Brieuc vs Paris 13 Atletico | 2.62 | 3.11 | 2.62 |
| 13. 20/01/23 | 21:30 | Villefranche Sur Saone vs Red Star | 2.66 | 3.21 | 2.52 |

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa, vodacom m-pesa, halopesa, airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ANCELOTTI: MADRID IPO KATIKA WAKATI MGUMU

**RIYADH, Saudi Aarabia**

CARLO Ancelotti amepuuzia mbali kuhusu Real Madrid kudhalilishwa kimchezo na Barcelona kwenye fainali ya Supercopa de Espana, lakini amekubali kuwa wako katika "wakati mgumu."

Barca walitawala mechi ya El Clasico mjini Riyadh Jumapili, wakitwaa taji lao la kwanza chini ya kocha, Xavi wakati waliposhinda mabao 3-1.

Kiungo mshambuliaji Gavi alikuwa kinara wa mchezo huo, akifunga bao la kwanza na kutoa asisti kwa Robert Lewandowski kabla ya mapumziko.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania mwenye umri wa miaka 18, pia alitengeneza bao la tatu kwa 'Blaugrana' hao kwenye Uwanja wa King Fahd, huku Karim Benzema akifunga bao la kufutia machozi.

Kocha Ancelotti baada ya mchezo huo alisema: "Si wakati muhimu, ni wakati mgumu na mgumu. Kawaida hutokea kwa msimu mmoja. Inaweza kurekebishwa kwa kujitolea kwa kawaida na mtazamo wa kawaida.

"Wachezaji lazima watambue hilo. Makosa haya ni rahisi kuepuka."

# Mudryk atua rasmi Chelsea

**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea imethibitisha kumnasa mchezaji aliyekuwa akilengwa kwa muda mrefu na Arsenal, Mykhailo Mudryk kutoka Shakhtar Donetsk kwa mkataba wa kuvutia unaodhaniwa kuwa wa zaidi ya pauni milioni 88.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, amesaini mkataba wa miaka nane na nusu kule Stamford Bridge.

Mudryk aliiambia tovuti ya klabu: "Nina furaha sana kusaini Chelsea. Hii ni klabu kubwa, katika ligi nzuri na ni mradi wa kuvutia sana kwangu katika hatua hii ya maisha yangu.

"Nina furaha kukutana na wachezaji wenzangu wapya na ninatarajia kufanya kazi na kujifunza chini ya kocha Graham Potter."

'Washikabunduki' hao walikuwa wakimfuatilia nyota huyo wa Ukraine kwa miezi mingi, huku makubaliano yakifikiriwa kufikiwa kati ya kambi hizo mbili kuhusu kila kitu isipokuwa ada ya mwisho ya uhamisho.

Na huku mazungumzo yakifikia mkwamo, 'The Blues' walichukua fursa kwa kumtuma mmiliki mwenza, Behdad Eghbali na Mkurugenzi wa Uhamisho wa Kimataifa, Paul Winstanley, kwenda Uturuki ambako Shakhtar wanafanya mazoezi kwa sasa.

Nia ya Chelsea kulipa bei kamili ilisababisha mazungumzo yaendelee haraka na kumwona Mudryk akisafiri kwenda London Magharibi kwa ndege binafsi ya klabu ili kukamilisha uchunguzi wa afya juzi usiku.



## HABARI MICHEZO

15,605/-

# TALIB ASIFU USAJILI MPYA SIMBA

**Na Saada Akida**

BAADA ya dirisha dogo la usajili kufungwa juzi usiku huku Simba ikiwatambulisha wachezaji wapya wawili, Jean Othos Baleke na Hemed Ismael Sawadogo, Kocha wa zamani wa Simba, Talib Hilal, amefunguka na kusema klabu hiyo imelamba dume kwa kuwa ni wachezaji wazuri na wataisaidia timu hiyo.

Simba imewatambulisha nyota hao kwa ajili ya kuongeza nguvu ndani ya kikosi cha timu hiyo kujiimarisha kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika hivyo kusajili jumla ya wachezaji wanne katika dirisha hili dogo, wengine wawili wakiwa ni Saido Ntibazonkiza na mshambuliaji Mohamed Musa kutoka Malindi FC ya Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili jana mchana kwa simu, Talib alisema kusajiliwa kwa wachezaji hao ni sahihi kwa sababu ya mapungufu ya kikosi hicho katika safu ya kiungo mkabaji na ushambuliaji.

Alisema ameiona Simba ikiwa inacheza na kuna baadhi ya wachezaji ikiwakosa akiwamo kiungo mkabaji (Sadio Kanoute na Mzamiru Yassin), timu inaonekana kuzidiwa na kuwapa wapinzani mwanya wa kupata ushindi.

"Ni wachezaji wazuri, viongozi wametatua tatizo la Simba lililowasumbua, lakini kuongezeka kwa Kocha Mkuu (Roberto Oliveira) kutasaidia kufanya vizuri kwa timu hiyo endapo wachezaji watatambua thamani ya nembo ya jezi ya Simba," alisema Talib.

"Sina mashaka na Simba kutetea ubingwa walioupoteza msimu uliopita kwani kuna nafasi kubwa ya kujituma na kushinda michezo 11 iliyosalia katika ligi kwa sababu soka ni mchezo wa makosa na lolote linaweza kutokea," alisema Talib ambaye kocha wa soka la ufukweni nchini Oman.

Aliwataka wachezaji wa Simba kujituma zaidi kwa kucheza kwa jihadi kwa sababu anaimani na timu hiyo kutwaa ubingwa na kufanya vizuri katika michezo ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayoanza Februari 11, mwaka huu.

**SHUKRANI...**



Gavana wa Lions Club International District 411C Tanzania, Mustansir Gulamhussein (kushoto) na Rais wa Rotary E-Club ya Masaki, Akash Shah (kulia), wakimkabidhi cheti cha shukrani, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Musa Hassan Zungu, baada ya kumalizika kwa mbio za hisani za kukusanya fedha kwa ajili ya kutoa huduma ya matibabu ya macho kwa Watanzania wenye matatizo hayo. Mbio hizo zilifanyika mwishoni mwa wiki katika viwanja vya Farasi vilivyoko Oysterbay, Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# DIRISHA LA USAJILI LIGI KUU LILIVYOFUNGWA

INATOKA UK. 24

straika Atupele Green pekee, Coastal Union ikiwachukua Yusuph Athumani kutoka Yanga, Yema Mwamba wa KK Homeboyz ya Kenya, winga Juma Mahadhi kutoka Geita Gold, Felly Mulumba na Justin Ndikumana kutoka Bandari FC ya Mombasa Kenya, pamoja na Omari Banda akiwa huru.

**#POLISI TANZANIA**

Polisi Tanzania imemaliza usajili wake kwa kuwaingiza mastraika, Kelvin Sabato na Daud Mbweni kutoka Singida Big Stars, Ibrahim Hilika akitoka Mafunzo FC na Mayala Nenock kutoka SM Sangabalende ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, pia kiungo mkabaji Mohamed Issa 'Banka' na Abdul Hamahama wote kutoka Namungo.

**#KMC FC**

Timu ya KMC imemzoa kipa wa Prisons, Hussein Abel, huku Singida Big Star ikiwasajili kina Fransis Kazadi, Brigh Adjei kutoka Aduana Stars ya Nigeria, Ibrahim Ajibu kutoka Azam FC, Yusuph Kagoma kutoka Geita Gold, Nickson, Kibabage wa Mtibwa Sugar, Marcos Silva kutoka Brazil, Kelvin Nashon, Geita Gold, Enock Atta wa Ghana.

**#MTIBWA, NAMUNGO, GEITA GOLD**

Kwa upande wa Mtibwa Sugar imemsajili Vitalis Mayanga kutoka Polisi Tanzania, huku Namungo ikimtwaa Frank Domayo akiwa huru na Miza Kiristom wa Mbeya Kwanza wakati Geita Gold ikimsajili Bashima Sauli Saite kutoka Mlandege.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 21/01/23 | 18:00 | AFC Bournemouth vs Nottingham Forest | 2.60 | 3.20 | 2.65 |
| 02. 21/01/23 | 18:00 | Southampton FC vs Aston Villa | 2.80 | 3.30 | 2.42 |
| 03. 21/01/23 | 18:00 | Birmingham City vs Preston North End | 2.38 | 3.10 | 3.10 |
| 04. 21/01/23 | 18:00 | Blackpool vs Huddersfield Town | 2.27 | 3.15 | 3.20 |
| 05. 21/01/23 | 18:00 | Cardiff City vs Millwall FC | 2.95 | 3.05 | 2.48 |
| 06. 21/01/23 | 18:00 | Queens Park Rangers vs Swansea City | 2.55 | 3.25 | 2.70 |
| 07. 21/01/23 | 18:00 | Wigan Athletic vs Luton Town | 2.75 | 3.15 | 2.55 |
| 08. 21/01/23 | 18:15 | Espanyol Barcelona vs Real Betis Seville | 2.80 | 3.15 | 2.55 |
| 09. 21/01/23 | 22:00 | SC Cambuur vs Sparta Rotterdam | 2.95 | 3.35 | 2.31 |
| 10. 21/01/23 | 23:00 | RKC Waalwijk vs Go Ahead Eagles | 2.36 | 3.45 | 2.80 |
| 11. 22/01/23 | 13:30 | Gaziantep FK vs Sivasspor | 2.50 | 3.30 | 2.75 |
| 12. 22/01/23 | 15:00 | Sunderland AFC vs Middlesbrough FC | 2.80 | 3.25 | 2.45 |
| 13. 22/01/23 | 16:30 | Feyenoord Rotterdam vs Ajax Amsterdam | 2.85 | 3.55 | 2.28 |
| 14. 22/01/23 | 17:00 | Leeds United vs Brentford FC | 2.39 | 3.45 | 2.75 |
| 15. 22/01/23 | 17:00 | AC Monza vs Sassuolo Calcio | 2.26 | 3.30 | 3.10 |
| 16. 22/01/23 | 18:30 | Maritimo Madeira vs Estoril Praia | 2.55 | 3.15 | 2.80 |
| 17. 22/01/23 | 19:30 | Borussia Monchengladbac vs Bayer Leverkusen | 2.70 | 3.80 | 2.31 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 17/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2773 | Sivasspor vs Bursa Niluferspor | 1.31 | 5.03 | 7.36 |
| 15:35 | 4639 | AL Arabi (SA) vs Al Qadisiyah | 2.22 | 2.87 | 3.31 |
| 15:45 | 3718 | Proodeftiki FC vs Episkopi FC | 2.12 | 2.86 | 3.59 |
| 15:55 | 3393 | Ohud Medina vs Hajer Club | 2.54 | 2.78 | 2.88 |
| 16:00 | 3418 | Singida BS FC vs Kagera Sugar | 1.63 | 3.46 | 5.07 |
| 16:25 | 4687 | Al Rayyan SC vs AL Wakrah | 3.31 | 3.55 | 1.94 |
| 16:30 | 2212 | Rajasthan United vs Churchill Brothers | 2.29 | 3.12 | 2.92 |
| 16:30 | 3247 | Cape Town All Stars vs Black Leopards | 1.77 | 3.07 | 4.77 |
| 16:30 | 4771 | JDR Stars vs Baroka FC | 2.04 | 2.92 | 3.75 |
| 16:30 | 5222 | Casric Stars FC vs Ajax Cape Town | 2.12 | 2.83 | 3.66 |
| 17:00 | 2229 | Sporting CP U23 vs Estoril Praia U23 | 3.07 | 3.51 | 2.04 |
| 17:30 | 5347 | Antalyaspor vs Kayserispor | 2.04 | 3.30 | 3.25 |
| 19:00 | 4857 | Al Sadd SC vs Lekhwiya SC | 2.21 | 3.75 | 2.63 |
| 19:00 | 5465 | Mozambique vs Libya | 3.65 | 2.95 | 2.19 |
| 20:00 | 2993 | Pafos FC vs Akritas Chlorakas | 1.13 | 6.79 | 15.53 |
| 20:30 | 2333 | Alanyaspor vs Galatasaray | 3.40 | 3.74 | 1.86 |
| 20:30 | 5325 | OH Leuven vs Eupen | 1.73 | 3.88 | 4.18 |
| 21:00 | 5213 | Real Sociedad vs Mallorca | 1.71 | 3.47 | 4.96 |
| 21:30 | 2089 | SAO Bento SP vs Santo Andre SP | 2.53 | 2.77 | 2.91 |
| 22:00 | 4681 | Algeria vs Ethiopia | 1.46 | 4.09 | 7.18 |
| 22:45 | 1055 | Wigan vs Luton Town | 2.91 | 3.16 | 2.36 |
| 22:45 | 1203 | Standard Liege vs Mechelen | 2.03 | 3.54 | 3.34 |
| 22:45 | 1225 | Ebbsfleet vs Chelmsford | 1.41 | 4.37 | 6.21 |
| 22:45 | 1327 | Hampton and Richmond vs Cheshunt | 1.90 | 3.46 | 3.51 |
| 22:45 | 1447 | Dundee FC vs Dunfermline | 1.70 | 3.80 | 3.99 |
| 22:45 | 1492 | Ballyclare vs Annagh Utd | 3.65 | 3.55 | 1.84 |
| 22:45 | 1728 | Marske United FC vs Liversedge | 2.01 | 3.64 | 3.06 |
| 22:45 | 1972 | AFC Fylde vs Buxton FC | 1.63 | 3.75 | 4.58 |
| 22:45 | 1981 | Wealdstone vs Oldham | 2.38 | 3.31 | 2.76 |
| 22:45 | 2355 | Corinthian Casuals vs Horsham | 3.50 | 3.95 | 1.89 |
| 22:45 | 2528 | Southport vs Boston Utd | 2.14 | 3.26 | 3.07 |
| 22:45 | 2684 | Solihull Moors vs Aldershot | 1.89 | 3.65 | 3.56 |
| 22:45 | 2920 | Altrincham vs Maidenhead U | 1.83 | 3.59 | 3.84 |
| 22:45 | 3213 | Poole Town vs Plymouth Parkway | 1.67 | 4.20 | 4.20 |
| 22:45 | 3467 | Forest Green vs Birmingham | 3.70 | 3.51 | 1.89 |
| 22:45 | 3601 | KVC Westerlo vs Racing Genk | 3.62 | 3.57 | 1.93 |
| 22:45 | 3851 | Wolverhampton vs Liverpool | 3.65 | 3.60 | 1.87 |
| 22:45 | 4576 | Accrington vs Boreham Wood | 1.96 | 3.40 | 3.55 |
| 22:45 | 4627 | Lewes vs Canvey Island | 2.33 | 3.70 | 2.70 |
| 22:45 | 4932 | Matlock Town vs South Shields | 2.72 | 3.35 | 2.31 |
| 22:45 | 5036 | Peterborough Sports vs Gloucester City | 2.04 | 3.35 | 3.21 |
| 22:45 | 5049 | Torquay vs Bromley | 2.80 | 3.59 | 2.22 |
| 22:45 | 5304 | Dagenham and Redbridge vs Eastleigh | 2.04 | 3.49 | 3.25 |
| 22:45 | 5443 | Barnet vs Yeovil | 1.89 | 3.51 | 3.70 |
| 22:45 | 5499 | Torquay vs Taunton Town | 1.89 | 3.45 | 4.00 |
| 22:45 | 5714 | Guiseley vs Lancaster City | 2.03 | 3.27 | 3.32 |
| 22:45 | 5957 | Swansea vs Bristol City | 1.96 | 3.45 | 3.50 |
| 23:00 | 2608 | Napoli vs Cremonese | 1.22 | 6.18 | 10.97 |
| 23:00 | 2710 | West Bromwich vs Chesterfield | 1.36 | 4.84 | 6.91 |
| 23:00 | 3815 | Alaves vs Sevilla FC | 3.98 | 3.39 | 1.89 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Januari 17, 2023
Nipashe




UKURASA 21

## Arteta aanza kuota ubingwa EPL Arsenal

# DIRISHA LA USAJILI LIGI KUU LILIVYOFUNGWA

## ●●●Simba, Yanga ni kishindo, nani katoka, kaingia timu zote 16, Talib Hilal asifu...

**Na Adam Fungamwango**

DIRISHA dogo la usajili kwa wachezaji wa ligi zote nchini lilifungwa juzi saa sita usiku, huku klabu zikifanikiwa kupata wachezaji ambao wanaona watazisaidia timu zao.

Saa tano usiku juzi, Simba ilimtangaza straika Jean Baleke aliyekuwa akichezea kwa mkopo Klabu ya Nejmeh ya Lebanon akitokea TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, na ilipotimu saa sita usiku Yanga ilitangaza kumsajili Mamadou Doumbia kutoka nchini Mali.

Ni kipindi ambacho klabu zilikuwa zinapigana vikumbo huku na huko kusaka wachezaji ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuviongezea nguvu vikosi vyao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**#SIMBA**

Imekamilisha usajili wa wachezaji wanne kwenye kipindi hiki cha dirisha dogo ambao ni Saido Ntibazonkiza kiungo mshambuliaji kutoka Geita Gold, straika Baleke (Nejmeh ya Lebanon), kiungo mkabaji Ismael Sawadogo (Difaa El Jadida ya Morocco) na straika chipukizi kutoka Malindi anayesemekana ni chaguo la Kocha Mkuu, Robertinho Oliveira.

**#YANGA**

Imefanya ingizo la wachezaji wanne ambao ni straika Kennedy Musonda kutoka Power Dyanamos ya Zambia, beki wa kati Doumbia (Stade Malien ya Mali), golikipa Metacha Mnata (Singida Big Stars) na Mudathir Yahaya ambaye alikuwa mchezaji huru.

**#AZAM, MBEYA CITY, DODOMA JIJI NA IHEFU**

Timu zingine zilizofanya usajili wake kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana kutoka vyanzo mbalimbali, pamoja na klabu zenyewe kuthibitisha ni Azam FC ambayo imemsajili kipa Abdulai Iddrisu kutoka nchini Ghana, Mbeya City ikimsajili kiungo James Msuva kutoka Singida Big Stars, Dodoma Jiji ikiwanasa Steven Sey, straika raia wa Ghana akiwa huru na Adeyum Salehe kutoka Geita Gold, Ihefu ikithibitisha kuwasajili mastraika wawili, Adam Adam kutoka Mtibwa Sugar na Mudathir Abdallah kutoka Prisons, pamoja beki wa kati David Mwantika kutoka Singida Big Stars.

Hata hivyo zipo taarifa ambazo hazijathibitishwa kuwa wachezaji wawili wa Simba, Nelson Okwa na Vicent Akpan, wamepelekwa Ihefu FC kwa mkopo ambapo pia inahusishwa kumsajili Yacouba Songne aliyeachwa na klabu ya Yanga.

**#PRISONS**

Prisons imesajili wachezaji watano, wanne wakiwa ni huru nao ni kipa Benedict Tinoco, straika Lambart Sabianka, viungo washambuliaji wawili, Shaaban Kisiga na Mohamed Ibrahim 'Mo', pamoja na Meshack Selemani kutoka Nyasa Big Bullets.

**#RUVU SHOOTING, COASTAL**

Ruvu Shooting imemsajili

INAENDELEA UK. 23

**KIMO...**



Kiungo wa Simba, Sadio Kanoute, akiucheza mpira kwa kichwa dhidi ya mchezaji wa CSKA Moscow ya Urusi katika mechi ya kirafiki iliyopigwa Falme za Kiarabu juzi na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2.

## Robertinho aona nuru Simba CAF

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya CSKA Moscow ya Urusi juzi kwenye Uwanja wa Sheikh Zayed jijini Abu Dhabi, Falme za Kiarabu, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, amesema kama wachezaji wake watakuwa kwenye kiwango kama hicho kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, basi hakuna timu ya kuwazuia.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kocha huyo alisema kwa siku tano tu alizokuwa na timu na aina ya soka walilocheza dhidi ya CSKA Moscow hasa kipindi cha pili, limemshangaza hata yeye mwenyewe, hivyo ameahidi kuzidi kurekebisha makosa aliyoyaona na kutengeneza kikosi bora, imara ambacho atakuwa amekimezesha falsafa yake kuelekea Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Nina furaha kwa sababu kikosi nimekifundisha kwa siku tano tu, lakini wachezaji wananielewa na wanaendelea kufanya vizuri. Kwa mimi kipindi cha pili kimekuwa kizuri sana, kimenishangaza sana kutokana na uwezo mkubwa waliouonyesha Simba na nimejaribu kuwapa nafasi wachezaji vijana, nikajaribu kutengeneza uwiano wa wachezaji wakongwe na mwanzo mzuri kuelekea kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kwa sababu tumecheza na timu kubwa si Ulaya tu bali duniani.

Wale vijana walioingia kipindi cha pili walibadilisha kabisa mpira, wakaanza kucheza mpira wa kasi kama falsafa yangu inavyotaka. Nataka kutetengeneza kikosi bora, imara na falsafa mpya kuelekea kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema kocha huyo.

Robertinho alisema anachokiona mbele kwa Simba ni mafanikio kwenye ligi hiyo kwa sababu kwanza Simba ni wazoefu kwenye michuano hiyo, hivyo haitowapa tabu sana, lakini pia ameisifu kambi ya Dubai kuwa imekuwa bora kwa kila kitu kuanzia hoteli yenyewe, vifaa vya mazoezi na hata vyakula.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >